# Nipashe

Ijumaa Juni 7, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579938

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wanandoa wadaiwa kuuawa kikatili ugomvi wa kifamilia

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**WAZIRI MPINA ALETA VIWANDA 15 MAZIWA**
UAMUZI uliofanywa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kudhibiti uingizaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi kupitia 'Operesheni Nzagamba'...

**UKURASA WA 3**


**JPM KUKUTANA NA WAFANYABIASHARA LEO**
RAIS John Magufuli leo atakutana na wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini na wajumbe wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC)...

**UKURASA WA 3**

**FAMILIA YAELEZA AFYA YA MAMA MARIA NYERERE**
HALI ya mke wa Baba wa Taifa, Maria Nyerere (88), inaendelea kuimarika baada ya kupatiwa matibabu nchini...


# NSSF yawasaka waajiri wakaidi

UKURASA 2




Askari wa doria ya pikipiki maarufu kama Tigo, akijaribu kumkamata mwendesha bodaboda kwa kumzuia na mguu wakiwa kwenye mwendo eneo la Hospitali ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Bil. 23/- kujenga soko la ghorofa

UKURASA 24

# Kibano chaja taasisi wadaiwa sugu ardhi

**LUKUVI** aziita Dodoma kujieleza, atishia kuzifutia umiliki kwa kushindwa kulipa kodi... *Endelea ukurasa wa 24*

MICHEZO — SAMATTA: TUTAFANYA MAKUBWA UK. 32 — MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Mimba za utotoni zaitikisa Kagera

**Na Lilian Lugakingira,** KARAGWE

WATOTO 2,527 wenye umri wa chini ya miaka 18, wamepata mimba za utotoni katika Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, katika kipindi cha mwaka jana.

Akizungumza katika kikao cha tathmini cha kampeni ya kupinga mimba za utotoni inayoratibiwa na Shirika la World Vision Tanzania, Kanda ya Kagera, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Godwin Kitonka, alisema idadi hiyo imeongezeka ikilinganishwa na watoto 1, 297 waliopewa ujauzito kwa mwaka 2017.

Kitonka alisema hali hiyo inaashiria kuwa kuna vijana na watu wazima wanaofanya ngono zembe na watoto.

"Hivi visingizio vya mtoto wa kike kumtaja mtu mwingine kuwa ndiye aliyempa mimba au kukataa kutaja aliyempa mimba eti hamjui vimepitwa na wakati. Ifike wakati vyombo vya usalama viwaminye ili wataje waliowapa mimba ili hatua zichukuliwe na iwe fundisho kwa watu wengine," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Owokusiima Kaihula, alitaja baadhi ya visababishi vya mimba hizo kuwa ni mila potofu za kuozesha watoto wadogo na baadhi ya wazazi kushindwa kutoa matunzo kwa watoto wao.

Naye mshiriki wa kikao hicho, Mchungaji Severine Selestine kutoka Kanisa la kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Usharika wa Omurushaka, alisema baadhi ya sababu za mimba za utotoni ni wafanyakazi wanaoletwa katika familia.

INAENDELEA UK.8



Wakazi wa jiji wakivunja sheria kwa kupita kwenye uzio wa chuma uliowekwa kuzuia watu wasipite katika Barabara ya Mandela, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, badala ya kupita kwenye daraja la juu lililojengwa na serikali ili kuepusha ajali kwa waenda kwa miguu. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# NSSF yaanza kuwasaka waajiri binafsi

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa kushirikiana na vyombo vya serikali na binafsi umeanza kuwasaka waajiri binafsi ambao wafanyakazi wao hawajaandikishwa.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alisema ni zoezi maalum litakalofanyika hadi mwezi Julai, mwaka huu.

"Sekta binafsi ni kubwa sana tunaendelea kuandikisha wanachama kwa kadiri tunavyowafikia, hadi sasa hatujawafikia wote kwa kuwa siyo waajiri wote wanaleta wanachama kwa hiyari," alisema.

Alisema lengo ni kuwafikia waajiri wote wa sekta binafsi ili kuhakikisha watu wote wa sekta binafsi wanachama wao wanaandikishwa na kupeleka michango NSSF.

"Siyo kila mwajiri analeta majina ya wafanyakazi wake, ili waandikishwe kuwa wanachama na alete michango, tumelibaini hilo sasa tunawatafuta kokote waliko ili watekeleze takwa la kisheria," alisema.

Alisema wameendelea kuandikisha wanachama wapya kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa mujibu wa sheria inayotaka sekta binafsi kuwa wanachama wa NSSF.

Alisema kati ya mwezi Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu, walisajili wanachama wapya 98,966 ikiwa ni asilimia 110 ya lengo.

**AINA YA WANACHAMA**

Alisema kuna wanachama wa aina mbili, walioajiriwa ni lazima wawe wanachama wa NSSF na wasipojiandikisha wanachukuliwa hatua.

Kundi jingine ni waliojiajiri ambao ni hiyari kujiunga na kupeleka michango, ambao kwa sasa NSSF imeandikisha mfumo maalum kwa Msimamizi na Mdhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), unaojulikana 'National Informal Sector Scheme'.

Alisema baada ya kukamilisha uanzishaji wa mfumo huo wameanza kuwasajili wanachama wa hiyari kwa kutumia mfumo huo.

"Tatizo kwa wanachama wa hiyari akiamua kujiunga leo anaingia na akiamua kutoka anatoka. Akitoka kabla hajakidhi vigezo vya mafao anarudishiwa michango yake...kubwa tunawahamasisha kuchangia na kubaki," alisema.

Erio alisema kwa uzoefu kwa mifuko yote ya hifadhi ya jamii, wanachama wa hiyari wanaojiandikisha ni asilimia 90, lakini wanaochangia ni asilimia 10, na hawawezi kuchukuliwa hatua yoyote kwa kuwa ni hiyari kujiunga.

"Tunataka kuwakuta kwenye vikundi, tunatumia gharama kuwafikia waliko na ndiyo maana tunawahamasisha kila wakati kwa kuwaeleza faida za hifadhi ya jamii," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, takwimu za nyuma zinaonyesha kuwa katika waajiriwa 100 kati yake 93 wako kwenye sekta binafsi.

"Kwa sababu ni takwa la kisheria, uwezo wa kuwasajili tunao na ndiyo maana tunaimarisha mifumo ya kielektroniki ili tuwasajili na kukusanya michango kielektroniki," alisema.

**CHANGAMOTO**

Erio alisema changamoto kubwa iliyopo sekta binafsi ni waajiri kupeleka michango kwa hiyari na kwa wakati na wengine kutotoa idadi sahihi ya wafanyakazi wao kwa mujibu wa sheria.

Alisema wengine wanaajiri wafanyakazi kwa masharti ya kutowaandikisha wala kupeleka michango yao na wengi hukubali kufanyakazi kwa kuwa wanachotaka ni mshahara pekee.

Alibainisha kuwa bado watu hawajatofautisha katika hifadhi ya jamii na benki na ndiyo maana kila siku wanakuja wanapokosa ada ya mtoto au kodi ya nyumba na kwamba hifadhi ya jamii inataratibu zao.

Erio alisema changamoto nyingine ni kwa wachangiaji wa hiyari ambao wengi kipaumbele ni kupata fedha ya kukidhi mahitaji ya wakati husika na siyo kwa mipango ya baadaye.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi Tarehe **8/5/2019** kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mizigo yake wenye vipimo vikubwa kama ifuatavyo;

A. Kutoka **KILOMBERO** kuelekea **SONGEA.** Gari lenye namba za usajili

**T875 CZT /T901 CZT**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.50 |
| Upana | - | mita | 2.70 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

B. Kutoka **NAMANGA** kuelekea **SONGEA.** Gari lenye namba za usajili **T339DEC/T364 DCF**

**Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.50 |
| Upana | - | mita | 2.90 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika **KILOMBERO** mpaka **SONGEA** Kupitia IRINGA
4. Njia itakayotumika NAMANGA mpaka **SONGEA** Kupitia **MOSHI**

Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

xxxxxx


# Operesheni ya Waziri Mpina yaleta viwanda 15 vya maziwa

**Na Mwandishi Maalum**

UAMUZI uliofanywa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kudhibiti uingizaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi kupitia 'Operesheni Nzagamba', umewezesha kutengeneza fursa ya kuanzishwa viwanda vipya 15 vya maziwa katika mwaka wa fedha 2018/ 2019 vyenye uwezo wa kusindika lita 90,400 kwa siku.

Hatua hiyo itaongeza soko la maziwa kwa wafugaji sambamba na kufungua fursa mpya za ajira kwa Watanzania na kuongeza mapato ya serikali kutokana na uanzishwaji wa viwanda hivyo vipya.

Operesheni Nzagamba inayofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalenga kuwalinda wazalishaji wa ndani, ajira za Watanzania na mapato ya serikali ambapo wawekezaji wengi waliogopa kuwekeza nchini kutokana na utitiri wa bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi zilizokuwa zinaingia nchini bila vibali, bila kukaguliwa ubora na bila kulipiwa tozo na kodi mbalimbali za serikali.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Dk. Sophia Mlote, alivitaja viwanda hivyo vipya 15 vilivyoanzishwa na mikoa vilipo kwenye mabano ni Galaxy Foods and Beverage wazalishaji wa maziwa ya 'Kilimanjaro Fresh' chenye uwezo wa kusindika

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA



Wachuuzi wa bidhaa wakifanyia biashara zao, kwenye kituo cha basi cha Magomeni Mikumi, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa abiria na kukosa sehemu ya kupumzikia wakati wakisubiri usafiri. **PICHA: JOHN BADI**

## Magufuli sasa kukutana na wafanyabiashara leo D'Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli leo atakutana na wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini na wajumbe wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC).

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, wafanyabiashara watano kutoka kila wilaya nchini watawawakilisha wafanyabiashara wenzao.

Ilisema mkutano huo utafanyika asubuhi Ikulu jijini Dar es Salaam.

# Wadaiwa kuuawa kisa ugomvi wa kifamilia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga, Manyara Ndelema (48) na mkewe Nyamizi Mserengeti (40), wameuawa kwa kuchinjwa shingoni kwa madai ya kuwapo migogoro ya mashamba ya kifamilia.

Inadaiwa kuwa Ndelema alinunua mashamba ya familia yao baada ya kuuziwa na wanafamilia ili wapate kumaliza matatizo yaliyokuwa yakiwaandama, lakini baada ya ndugu zake hao kukosa mahali pa kulima, waliibua mgogoro kuyataka mashamba hayo na kusababisha mauaji yake pamoja na mkewe.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, jana aliwaambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Juni Mosi, mwaka huu, majira ya saa 7:00 usiku.Alisema Ndelema akiwa amelala na mkewe, walivamiwa na watu na kisha kukatwa maeneo ya miili yao ikiwamo shingo na mabega.

Alisema baada ya mauaji hayo, wahusika walikimbia kusikojulikana na Jeshi la Polisi lilifanya msako mkali na kuwakamata wawili na baadaye kuwakamata watuhumiwa wengine wanne juzi Nzega mkoani Tabora.

"Chanzo cha mauaji ya watu hawa mume na mke ni ugomvi wa mashamba ya kifamilia, ambayo waliyanunua kutoka kwa ndugu zao waliokuwa wakikabiliwa na shida mbalimbali. Baada ya kuyanunua ndugu hao walianza kuyataka kwa nguvu baada ya kukosa maeneo ya kulima, hivyo kuamua kuwaua ili wapate kuyamiliki tena," alisema Abwao.

"Miili ya marehemu tumeikabidhi kwa ndugu zao wengine kwa ajili ya taratibu za mazishi baada ya daktari wa serikali kumaliza kuifanyia uchunguzi, ili wapate kupumzishwa kwenye makao yao ya milele," aliongeza.

Aidha, alisema watuhumiwa hao sita baada ya taratibu za kiupelelezi kukamilika, watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

## Hali ya mama Maria Nyerere yaimarika

**Na Salome Kitomari**

HALI ya mke wa Baba wa Taifa, Maria Nyerere (88), inaendelea kuimarika baada ya kupatiwa matibabu nchini.

Msemaji wa Familia, Makongoro Nyerere, aliiambia Nipashe kuwa Mama Nyerere bado anaumwa, lakini anaendelea vizuri.

"Anaumwa, amelezwa Hospitali ya Mzena, Kijitonyama na anaendelea vizuri," alijibu Makongoro.

Mama Nyerere aliugua akiwa nchini Uganda, kuhudhuria ibada maalum ya kumbukumbu ya mashahidi wa Uganda eneo la Namugongo, Juni 3, mwaka huu.

Alitarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye sherehe hizo na Rais Yoweri Museveni alishindwa kuhudhuria kwa kuwa alikwenda kumtembelea hospitalini jijini Kampala.

Aidha, taarifa zinaeleza Rais Museveni alimtuma mwakilishi kwenye tukio la siku ya mashahidi wa Uganda ili kuwaepusha waumini kusubiri kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa BBC Swahili, Mama Nyerere alisindikizwa hadi Uwanja wa Ndege wa Entebbe, kupanda ndege ya kurudi nchini kwa ajili ya matibabu zaidi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa aliondoka uwanjani humo kwa ndege maalum aliyopewa na Rais wa Uganda, Museveni, kuelekea jijini Dar es Salaam kwa matibabu zaidi.

Mama Nyerere alipata matatizo ya kiafya usiku kabla ya tukio la kumkumbuka mumewe Mwalimu Julius Nyerere kama aliyewasaidia mashahidi wa Uganda.

RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz @RadioOneStereo @RadioOneStereo @radioonetz

# Wahitimu wafundishwa ujasiriamali wa kilimo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAHITIMU wa vyuo vikuu waliomaliza shahada ya kilimo na kukosa ajira, wamewezesha kupatiwa mbinu na mafunzo ya ujasirimali ili kutumia elimu yao kujiajiri kupitia sekta hiyo.

Mafunzo hayo yanafanywa kupitia mpango wa mradi wa Kituo Atamizi cha Kilimo Biashara kilichoko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi Binafsi ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (PASS) kwa ufadhili wa Serikali ya Denmark.

Kwa kuanza, mradi huo umewapa mafunzo wahitimu 20 ili wakimaliza waende kujiajiri badala ya kutegemea ajira.

Akizungumza juzi mbele ya Balozi wa Denmark, Meneja wa Mradi huo, Richard Bruno, alisema kupitia mpango huo wahitimu hao wanafundishwa kilimo biashara cha nyanya na tayari wamejipatia Sh. milioni 15 kutokana na mavuno ndani ya miezi minne.

Alisema kiasi hicho kimetokana na mavuno ya kuanzia Februari hadi Mei, mwaka huu, mafanikio ambayo yanahamasishwa na serikali ya awamu ya tano.

Naye Balozi wa Denmark nchini Tanzania, Einar Jensen, ambaye alitembelea mradi huo huo, alisema lengo lao ni kuhakikisha wahitimu hao wa kilimo wanatumia taaluma yao ili kuongeza tija katika uzalishaji wa chakula nchini.

Alisema ili kuongeza uzalishaji wa kilimo nchini wameamua kuwasaidia wahitimu wa kilimo, ili kutumia taaluma walizozipata kusaidia kuendesha kilimo cha kisasa kwa kuanzia na kilimo cha nyanya ambacho kwa sasa kina soko kubwa.



Wachuuzi wa maua ya zawadi wakiyaandaa kabla ya kuyauza, kando ya Barabara ya Haile Selassie jirani na Kanisa Katoliki la Mt. Peter, eneo la Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mtoto afungua kesi kutaka urithi wake

**Na Hellen Mwango**

MARY Nyaronga amefungua kesi ya mirathi Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Dar es Salaam akiomba iwaamuru wasimamizi wa mirathi ya marehemu baba yake, John Nyaronga, wampatie urithi wake.

Kesi hiyo ya mirathi namba 266/2019, imepangwa kusikilizwa Septemba 11, 2019, mbele ya Jaji Dk. Atuganile Ngwala.

Kwa mujibu wa hati ya mirathi hiyo, wasimamizi ambao pia ni walalamikiwa katika kesi hiyo, ni Dk. George Nyaronga, Anna Nyaronga, Bahati Kivugo (mke wa marehemu) na Denis Arego ambaye ni mtoto wa marehemu aliyejitokeza baada ya baba yake kufariki dunia.

Wakati mtoto huyo akidai haki yake, mahakama hiyo imetoa zuio la kutokuuzwa kwa hoteli ya marehemu Nyaronga iliyoko Musoma mkoani Mara mpaka kesi ya msingi iliyoko mahakamani itakaposikilizwa.

Uamuzi huo ulitolewa mwanzoni mwa wiki na Jaji Dk. Ngwala, wakati kesi hiyo ilipopangwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kusikilizwa. Zuio hilo lilitolewa baada ya malumbano ya pande zote mbili.

Jaji Ngwala aliwataka upande wa walalamikiwa ndani ya siku 14 kuwasilisha kiapo kinzani mahakamani hapo na watatakiwa kukiwasilisha Juni 18, mwaka huu.

Alisema kama kutakuwa na majibu yoyote kutoka kwa mlalamikaji (Mary) kutokana na kiapo kinzani kitakachowasilishwa na walalamikiwa, naye atatakiwa kuyawasilisha Juni 26, mwaka huu. Mary anawakilishwa na Wakili John Laswai.

Mary alifungua kesi hiyo, kuiomba Mahakama iwaamuru walalamikiwa kumlipa mali za urithi alizogawiwa baada ya baba yake kufariki dunia. Anadai kuwa mali hizo hajagawiwa tangu mwaka 2013.

Mlalamikaji (Mary) ameziainisha mali hizo katika hati yake ya kiapo aliyoiwasilisha mahakamani kuunga mkono maombi yake ya kutaka alipwe mali alizoachiwa na baba yake.

Mali hizo ni shamba la ekari tatu lililoko Kizito Huonjwa, kijiji cha Kimbiji Beach, shamba namba 2753, Kisanga kijiji cha Kisarawe lenye ekari 14, Injini ya boti iliyoko Chetah. Fedha Sh. milioni 15 kutoka benki ya NMB, Sh. milioni 22 kutoka katika hisa za Kampuni ya Meli ya Mediterranean (MSC) na shamba ekari 1.2 lililoko Kijiji cha Buganjo.

Mbali na mali hizo, Mary anadai alipewa pia nyumba iliyopo Mbezi Beach Africana ili wamiliki pamoja na Eva John ambaye ni ndugu yake, lakini hadi sasa hajapata fedha za pango za nyumba hiyo kwa sababu imepangishwa.

Mlalamikaji anaomba pia Mahakama iwaamuru wampe kiwanja ambacho kiko Misugusugu na nyumba aliyopewa iliyoko Musoma ambayo atamiliki pamoja na Anna na Emmanuel Nyaronga.

Walalamikiwa hao waliteuliwa kuwa wasimamizi wa mali za marehemu na Mahakama Kuu Oktoba 4, 2012 katika maombi ya mirathi namba 4/2012.

Baada ya kuteuliwa, Februari 18, 2013 wasimamizi hao waliwasilisha mahakamani hapo hati ya mgawanyo wa mali za marehemu kwa warithi wake wote.




TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +255 262 963309/13/14
Nukushi: +255 262 963 316
Barua pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz

Barabara ya Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Ghorofa ya Sita,
S. L. P. 2908,
40477DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA
### WITO WA KIKAO CHA WAZIRI WA ARDHI NA WAKUU WA TAASISI/MASHIRIKA NA MAKAMPUNI YANAYODAIWA KODI YA PANGO LA ARDHI

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anazitangazia Taasisi na Mashirika ya umma, Makampuni ya umma na binafsi pamoja na wenye maeneo ya viwanda na biashara yanayodaiwa kodi ya pango la ardhi na yenye malimbikizo ya muda mrefu kuhudhuria kikao maalum cha Mhe. William V. Lukuvi (Mb), Waziri wa Ardhi siku ya Jumanne tarehe 11 Juni, 2019 katika ukumbi wa Hazina, Dodoma kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi.

Mashirika, Taasisi na Makampuni yanayodaiwa kodi hii ya pango la ardhi na malimbikizo yanapaswa kufika yakiwa na nyaraka za umiliki pamoja na stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika. Aidha, wadaiwa watakaoshindwa kufika kwenye kikao hiki, hatua za kufuta milki zao na kuuza viwanja husika zitafuata kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (Sura 113) kifungu cha 50. Majina ya Taasisi, Mashirika na Makampuni husika yameorodheshwa katika website ya Wizara www.lands.go.tz. Kwa wadaiwa wengine, Ofisi zote za ardhi nchi nzima zitakuwa wazi siku zote pamoja na siku za Jumamosi na Jumapili hadi tarehe 30 Juni 2019 kwenda kuhakiki na kulipa.

Dorothy S. Mwanyika
KATIBU MKUU
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
5 Juni, 2019

1. AFRI BOTTLERS LTD
2. AFROIL INVESTMENT LIMITED
3. AGAKHAN FOUNDATION
4. AIR TANZANIA CORPORATION (ATC)
5. AKO GROUP CATERING SERVICE
6. ARUSHA INTERNATIONAL CONFERENCE CENTRE (AICC)
7. BOARD YA PARETO
8. BP TANZANIA LTD - PUMA ENERGY
9. BUGANDO MEDICAL CENTER
10. CABLA INVESTMENT COMPANY LTD
11. CARGILL TANZANIA LIMITED
12. CASHEWNUT BOARD OF TANZANIA
13. CF BUILDERS LIMITED
14. CHIEF COURT ADMINISTRATOR THE JUDICIARY OF TANZANIA
15. CHUO CHA MADINI DODOMA
16. CHUO CHA USHIRIKA MOSHI (MUCCOBS)
17. COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION
18. CONSOLIDATED HOLDING COOPORATION-TR
19. CRDB BANK PLC
20. D4N COMPANY LIMITED
21. DAR ES SALAAM MARITIME INSTITUTE
22. DAR ES SALAAM WATER & SEWERAGE AUTHORITY (DAWASA)
23. DODOMA URBAN WATER AND SEWARAGE AUTHORITY (DUWASA)
24. EAST AND SOUTHERN AFRICA MANAGEMENT INSTITUTE (ESAMI)
25. EFATHA MINISTRY
26. ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (EWURA)
27. ESTA BIDDING LIMITED
28. EXIM BANK TANZANIA LIMITED
29. EXPORT PROCESSING ZONE AUTHORITIES (EPZA)
30. FOOD SOL COMPANY LTD
31. GAPCO TANZANIA LIMITED
32. GAPOIL TANZANIA LTD
33. GOVERNMENT EMPLOYEES PROVIDENT FUND - PSSSF
34. GULF PETROLEUM (T) COMPANY LTD
35. HAWTE INVESTMENT
36. HEALTH OPERATIONS TANZANIA LTD
37. HIFADHI BUILDERS LTD
38. IJHUMILAGHA ASSOCIATES COMPANY LTD
39 IMMUNAL LABORATORY MEDICAL SUPPLY LTD
40. INSTITUTE OF ADULT EDUCATION
41. INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING
42. KAHAMA CO-OPERATIVE UNION LIMITED
43. KAHAMA MINING CORPORATION LTD
44. KAHAMA OIL M. LTD
45. KAMAL ALLOYS LTD
46. KARIAKOO MARKET CORPORATION
47. KIBAHA EDUCATION CENTRE
48. KIBENA TEA COMPANY LTD
49. KILOLO TEA COMPANY
50. KITANGARI TEACHERS COLLEGE
51. KITULO DIARY FARM - MINISTRY OF LIVESTOCK
52. KIZOTA AGRO PRODUCTS LTD
53. KOBIL TANZANIA LTD
54. LAKE OIL LTD
55. LAKE SECONDARY SCHOOL
56. LOCAL AUTHORITIES PENSIONS FUND - PSSSF
57. M.M.INTERGRATED STEEL MILLS LTD
58. M/S MARA CO-OPERATIVE UNION (1984) LIMITED
59. M/S MUSLIM UNIVERSITY OF MOROGORO
60. M/S TANZANIA FOOD, NUTRITION CENTRE
61. MALAMBUGI ENGINEERING COMPANY LTD
62. MARA REGION TRADING COMPANY
63. MARUNGU FARM
64. MATEBETE CHIMALA CATTLE BRANCH LTD
65. MBEYA CEMENT CO. LTD
66. MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY (MUST)
67. MBINGA COFFEE CURING COMPANY LTD
68. MBOZI MAIZE FARM LTD
69. MC OIL COMPANY LTD
70. MEDICAL STORES DEPARTMENT (MSD)
71. MEIS INDUSTRIES COMPANY LIMITED
72. MESSRS LAKE CHALA SAFARI LODGE LTD
73. MESSRS NDOLELA AFRICAN PLANTATION
74. MINERAL SEARCH OF AFRICA (TANZANIA LTD)
75. MOHAMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED
76. MOSHI MUNICIPAL COUNCIL
77. MOSHI URBAN WATER AND SEWARAGE AUTHORITY (MUWASA)
78. MOUNT MERU COMPANY
79. MSAMVU PROPERTY
80. MUFINDI PAPER MILLS
81. MUFINDI TEA COMPANY (DL)
82. MUSOMA DAIRY LIMITED
83. MUSOMA HOUSING DEVELOPMENT COMPANY
84. MUSOMA TEXTILE LIMITED
85. MWENGE UNIVERSITY
86. MZUMBE UNIVERSITY
87. NADAKA HOLDINGS LIMITED
88. NAFCO (MSAJILI WA HAZINA)
89. NATIONAL BANK OF COMMERCE LTD (NBC)
90. NATIONAL BOARD OF ACCOUNTANCY
91. NATIONAL COLLEGE OF TOURISM
92. NATIONAL DEVELOPMENT CORPORATION (NDC)
93. NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)
94. NATIONAL EXAMINATION COUNCIL (NECTA)
95. NATIONAL FOOD RESERVE AGENCY (NFRA)
96. NATIONAL HEALTHY INSURANCE FUND (NHIF)
97. NATIONAL HOUSING CORPORATION (NHC)
98. NATIONAL INSUARANCE CORPORATION (NIC)
99. N ATIONAL MEDICAL RESEARCH INSTITUTE (NMRI)
100. N ATIONAL MILLING CORPORATION (TR)
101. NATIONAL MUSEUM OF TANZANIA
102. NATIONAL RANCHING COMPANY LTD (NARCO)
103. NATIONAL SERVICE CORPORATION SOLE (SUMA JKT)
104. NATIONAL SHIPPING AGENCIES COMPANY LTD (TR)
105. NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND (NSSF)
106. NELSON MANDELA INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY
107. NEW TABORA TEXTILE
108. NIDA TEXTILES LTD
109. NORTH ZONE IRRIGATION AUTHORITY
110. NSAGALI COMPANY LTD
111. NYANZA COOPERATIVE UNION
112. OIL COM
113. ORYX OIL COMPANY LTD
114. PANAFRICAN CONSULTING AND EXPORTING TANZANIA
115. PARASTATAL PENSION FUND (PPF) - PSSSF
116. PHANTOM OIL TANZANIA LIMITED
117. PREVENTION AND COMBATING CORRUPTION BUREAU (PCCB)
118. PRIME AUTOMOBILE GARAGE AND SERVICE
119. PRIME REGIONAL SUPPLIERS LTD
120. PRIMEFUELS TANZANIA LIMITED
121. PUBLIC SERVICE PENSION FUNDS - PSPF
122. REGISTERED TRUSTEES OF EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH OF TANZANIA
123. REGISTERED TRUSTEES OF ROMAN CATHORIC
124. RELI ASSETS HOLDING COMPANY (TRC)
125. RIFT VALEY CO OPERATIVE UNION LTD (RIVACU)
126. ROBANDA VILLAGE COUNCIL
127. RUBADA - WIZARA YA KILIMO
128. RURAL ENERGY AGENCY (REA)
129. RWANDA EMBASSY
130. SAO HILL LTD
131. SERENGETI DISTRICT COUNCIL
132. SHINYANGA REGIONAL COOPERATIVE UNION (SHIRECU)
133. SMALL INDUSTRIES DEVELEOPMENT ORGANIZATION (SIDO)
134. SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE (SUA)
135. SONGWE WATER COMPANY LIMITED
136. SOUTHERN HIGHLAND BOTTLERS
137. ST. AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA (SAUT)
138. SUGAR BOARD OF TANZANIA
139. SUMBAWANGA AGRICULTURAL AND ANIMAL FOOD INDUSTRIES
140. TABORA TOBACCO PROCESSORS
141. TABORA URBAN WATER AND SEWARAGE AUTHORITY (TUWASA)
142. TANZANIA LOCAL GOVERNMENT WORKERS UNION (TALGWU)
143. TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD (TANESCO)
144. TANGANYIKA AGRICULTURAL SOCIETY
145. TANGANYIKA PACKERS LTD
146. TANGANYIKA WATTLE COMPANY LTD
147. TANTRADE (BOARD OF EXTERNAL TRADE)
148. TANZANIA POSTAL BANK (TPB)
149. TANZANIA AGRICULTURAL SOCIETY ORGANISATION (TASSO)
150. TANZANIA AIRPORTS AUTHORITY (TAA)
151. TANZANIA ASSEMBLES OF GOD
152. TANZANIA AVIATION AUTHORITY
153. TANZANIA BREWARIES LTD (TBL)
154. TANZANIA BUILDING AGENCY (TBA)
155. TANZANIA BUREAU OF STANDARDS (TBS)
156. TANZANIA COFFEE BOARD
157. TANZANIA COMMISSION FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY
158. TANZANIA COTTON AUTHORITY
159. TANZANIA COTTON LINT & SEED BOARD
160. TANZANIA DIARY FARMING
161. TANZANIA FERTILIZER COMPANY LTD
162. TANZANIA FISH RESEARCH INSTITUTE
163. TANZANIA FISHERIES CORPORATION
164. TANZANIA FOREST RESEARCH INSTITUTE
165. TANZANIA FOREST SERVICES (TFS)
166. TANZANIA INDUSTRIAL RESEARCH AND DEVELOPMENT ORGANISATION (TIRDO)
167. TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY (TIA)
168. TANZANIA INVESTMENT BANK (TIB)
169. TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC)
170. TANZANIA KOLPONG SOCIETY
171. TANZANIA LEAF TOBACCO COMPANY LTD
172. TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE (MPWAPWA)
173. TANZANIA METEOLOGICAL AGENCY (TMA)
174. TANZANIA MOZAMBIQUE CENTRE FOR FOREIGN RELATIONS (CFR)
175. TANZANIA NATION ROADS AGENCY (TANROADS)
176. TANZANIA NATIONAL PARKS
177. TANZANIA OXYGEN LTD
178. TANZANIA PETROLEUM DEVELOPMENT CORPORATION (TPDC)
179. TANZANIA PORTS AUTHORITY (TPA)
180. TANZANIA POSTS CORPORATION (TPC)
181. TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE
182. TANZANIA RAILWAYS CORPORATION (TRC)
183. TANZANIA REVENUE AUTHORITY (TRA)
184. TANZANIA SISAL BOARD
185. TANZANIA TEACHERS COLLEGE (TTC) MPWAPWA
186. TANZANIA TELECOMMUNICATION COMPANY (TTCL)
187. TANZANIA TIMBER MARKETING CO. LTD
188. TANZANIA TOBACCO EXPORTERS LIMITED
189. TANZANIA TROPICAL PESTICIDE RESEARCH INSTITUTE
190. TARIME RURAL DEVELOPMENT TRUST FUND
191. TANZANIA ELECTRICAL MECHANICAL AND ELECTRONICS SERVICES AGENCY (TEMESA)
192. TEOFIL KISANJI UNIVERSITY
193. THE BANK OF TANZANIA (BOT)
194. THE CEREALS AND OTHER PROCESS BOARD OF TANZANIA - WIZARA YA KILIMO
195. THE GOVERNMENT PROCUREMENT SERVICE AGENCY (GPSA)
196. THE NATIONAL MICROFINANCE BANK LIMITED (NMB)
197. THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA (OUT)
198. THE UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM (UDSM)
199. THE VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY (VETA)
200. TOBACCO AUTHORITY OF TANZANIA (TTB)
201. TOTAL TANZANIA LTD
202. TPSC MTWARA
203. TANZANIA UNION OF GOVERNMENT AND HEALTH EMPLOYEES (TUGHE)
204. TUMAINI UNIVERSITY
205. UYOLE AGRICULTURAL CENTER
206. WORLD FOOD PROGRAMME
207. ZONAL IRRIGATION UNIT

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuchangamkie fursa Kiswahili nje ya nchi

**LUGHA** ya Kiswahili ni fursa, ambayo Watanzania hawajaichangamkia ipasavyo kama inavyostahili.

Tunasema hivyo kwa kuwa mahitaji yake yanazidi kuongezeka kila uchao katika nchi za bara la Afrika hususan Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Kukua na kupanuka kwa lugha ya Kiswahili na kusababisha mahitaji ya wataalamu wa kuifundisha, kumezifanya nchi kadhaa kuchangamkia fursa hiyo kwa kuandaa kuzalisha wataalamu wake kwenda kufundisha nje ya nchi zao.

Kuna mifano kadhaa inayoonyesha hivyo. Kwa mfano, baadhi ya nchi za Afrika Mashariki licha ya kutotumia lugha hiyo kama lugha rasmi, lakini raia wake wengi wanajipenyeza katika nchi nyingine zinazowahitaji wataalamu wa kuifundisha.

Kimsingi, Tanzania ambako Kiswahili kinazungumzwa na wananchi wote na ni lugha rasmi, raia wake hawajaichangamkia fursa ya kwenda kufundisha lugha hiyo ng'ambo ambako mahitaji ni makubwa.

Kuna vyuo vikuu na taasisi nyingi za elimu katika nchi kadhaa kama Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchi za kusini mwa Afrika kama Afrika Kusini, Zimbabwe, Namibia, Zambia, Malawi, Botswana na nyingine, ambazo wataalamu wetu wangechangamkia kwenda kufundisha Kiswahili.

Licha ya kuchelewa kuchangamkia fursa hiyo, lakini muda bado upo na ni sasa kutokana na mahitaji makubwa, hivyo tunashauri zichukuliwe hatua mbalimbali za kuwezesha watu wetu kuziomba nafasi hizo kwa kuwa zina manufaa mengi kwao binafsi na taifa, yakiwamo ajira na pato lao kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu.

Limekuwa jambo zuri kutokana na Rais John Magufuli kufungua njia hiyo kwa kuonyesha mfano alipofanya ziara rasmi ya kikazi katika nchi za Afrika Kusini, Namibia na Zimbabwe hivi karibuni. Rais Magufuli aliwakabidhi viongozi wakuu wa mataifa hayo vitabu kadhaa vya lugha ya Kiswahili pamoja na kamusi. Hatua hiyo ya Rais ni kuitangaza lugha ya Kiswahili nje ili iwe sehemu ya fursa za kulinufaisha taifa letu.

Tunampongeza sana na tunawashauri viongozi wengine, wawakilishi wetu nje na Watanzania kwa ujumla kukitangaza Kiswahili wanapokuwa ughaibuni kwa lengo la kuwafanya watu wa nje kuelewa kuwa wanaweza kuwapata wataalamu wa lugha hiyo kutoka Tanzania.

Jitihada nyingine za kutia moyo katika kuchangamkia fursa za nje, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limetaja mikakati yake ya kuandaa wasomi wa kufundisha lugha hiyo nje, ikiwamo kuandaa kanzidata ya wanataaluma wote wa Kiswahili nchini na kuwapa mafunzo maalum.

Akizungumza na gazeti hili juzi msemaji wa Baraza hilo, Consolata Mushi alisema kanzidata hiyo itasaidia kuwatambua wanataaluma wote wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo nje ya nchi ili kuwaweka tayari kwa fursa hizo.


Kwa mujibu wa Bakita, awali zilikuwa zikija fursa moja moja, hivyo sasa wanaandaa kanzidata ya kuwatambua wanataaluma wote wa Kiswahili, ili iwe rahisi zinapokuja fursa pawapo na utaratibu mzuri.

Mkakati wa Bakita kuandaa wataalamu ni mzuri, isipokuwa uende sambamba na jitihada nyingine za ziada, ikiwamo kushirikiana na kufanyakazi pamoja na vyuo vikuu nchini ambavyo vinafundisha lugha ya Kiswahili na vina taasisi za kuendelea lugha hiyo kikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.


Pia njia nyingine ni Bakita na vyuo vyetu vikuu kwenda katika vyuo vya nje kufanya ushawishi ili viwape fursa za ajira wataalamu kutoka nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Mifuko plastiki imeondoka, vifungashio pia haviko sawa

**TAREHE** Mosi iliyopita, ndio ilikuwa mwanzo wa marufuku kwa matumizi ya mifuko ya plastiki Tanzania Bara, ambayo sasa iko kisheria. Wenzetu Zanzibar wanayo muda mrefu.

Kutokana na kupigwa marufuku mifumo hiyo, serikali ilitoa matangazo na kutaka uwepo mifuko mbadala kwa ajili ya kubebea bidhaa hizo.

Hivyo basi, watu wamechangamkia fursa hizo kwa kutengeneza mifuko mbadala kama ilivyoagizwa na serikali.

Mifuko ya plastiki inajulikana kuwa na madhara makubwa kiafya. Inaelezwa hata ikifukiwa haiozi na panapofanyika kilimo cha mazao, nayo haiozi.

Vivyo hivyo, inapoliwa na mnyama, haisagiki katika mfumo wa mwili wa mwanadamu, nayo katika hatua hiyo anadhurika.

Tumeona katika mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wamekuwa wakihamasisha watu kujiunga katika makundi, ili waweze kupata elimu ya kutengeneza mifuko mipya mdadala.

Kimsingi, tunapongeza juhudi hizo, kwani ni fursa ya kumuongezea mjasiriamali mdogo kipato cha ziada katika hilo.

Pamoja na kutengeneza kwa mifuko mbadala na kuinogesha kwa rangi maridhawa, tunaomba ubora uzingatiwe kutokana na pesa inayotumika kununua mfuko huo kubwa.

Bei mpya sasa ni kati ya Sh. 400 hadi Sh.1000, nasikitika kusema kupitia ushuhuda wa siku hizi chache tumegundua baadhi ya mifuko hifai, licha ya kuwa na rangi bora, japo ipo sokoni.

Unakuta mfuko unawekewa bidhaa, unachanika kabla ya kuanza safari. Sasa hapo ni kumtia hasara aliyenunua vitu.

> **Bei mpya sasa ni kati ya Sh. 400 hadi Sh.1000, nasikitika kusema kupitia ushuhuda wa siku hizi chache tumegundua baadhi ya mifuko hifai, licha ya kuwa na rangi bora, japo ipo sokoni. Unakuta mfuko unawekewa bidhaa, unachanika kabla ya kuanza safari.**

Inatakiwa wazalishaji waboreshe mifumo yao ili kuunguze malalamiko ya wateja. Nimtetee muuzaji katika hilo, hana kosa ndani ya wiki hii moja ya biashara mpya. Tukisema kosa namkosaji, moja kwa moja lipo kiwandani kwa wazalishaji.

Hiyo ni kwa sababu, tena katika mwanzo huu hatujui wazalishaji mifuko hiyo walilenga mbebaji wa vitu gani, hata kufikia isichanike kirahisi.

Ukienda madukani, hata uthabiti wa mifuko hiyo ukiwekewa soda, basi hata chupa mbili huwezi kuuning'iniza. Inabidi uikumbatie, maana ukining'iniza, hufiki mbali na chupa hizo, lazima zitaanguka na kupasuka.

Tunayapenda mabadiliko haya. Ila wazalishaji wa mifuko hii mipya waache kulipua. Tutengenezeeni vile yenye viwango.

Nihamie kwa marafiki zangu wa magengeni. Mnatumia bahasha za kuhifadhia pesa kuwekea wateja vitunguu na nyanya. Kweli huo ni mfuko mbadala? Ni mazingira nayo mnatakiwa kujiongeza katika magenge yenu.

Haya, nao wale wauza chipsi mlo wa wakazi wa mjini na vijana. Unapouza foili au 'take away' sio kuwawekea wateja wa chips katika mifuko ya kaki au magazeti.

Unakuta mteja anawekewa chipsi zinamafuta alafu anawekewa katika mfuko wa kaki au gazeti kwa kiafya sio sahihi.

Wauza chipsi wanatakiwa kujiongeza kuna wateja ambao wanatoka maeneo ya hapo jirani hawa nirahisi kuwa na kifaa cha kubebea na kuna wapita njia hawa wamekuta chipsi na wanataka kuondoka nazo, eti unamfungia katika gazeti au unaweka katika mfuko wa kaki, hii haipendezi.

## BARUA/MJADALA

# Tuwaenzi daima wagunduzi

**Mhariri,**

*NISEME wagunduzi wa vyuo vikuu nchini wanastahili sifa kwa kazi zao za ubunifu. Namuunga mkono Rais Dk. John Magufuli, kwa uongozi wake makini, alipotamka mambo yetu yasibakie kwenye makaratasi pekee.*

*Inakuwa vyema vijana wetu waliojitahidi kusoma vitabu vya kuwawezesha kugundua, stadi zao wanapaswa kufanyiwa kazi, kuenziwa na daima isiachwe hivi hivi, wahusika watakata tamaa, kwa kusema serikali haitujali.*

*Basi, maendeleo yetu yana uwezekano kuwa yatakwama hata kubakia maneno yasiyo na vitendo. Hivyo, wataalamu watakuwa na moyo kama serikali itasimamia ujuzi wao. Hayo ndio mafanikio yatakayoonekana na si jambo la kufanyia mchezo wa kuigiza.*

*Tuendelee vizuri kuwaenzi wataalamu wetu, kwani hakuna mtu atakayetufanyia kazi hii, ni sisi wenyewe. Lengo la rais wetu ni zuri sana, hawataki wavivu na walaza maendeleo, anawapenda wachapa kazi kama wale niliowaona katika Chuo Kikuu cha Dar as Salaam, wameonyesha ujuzi wao wote, katika maonyesho yao ya utafiti.*

*Naamini watakuwa walimu kwa wenzao walioko masomoni katika ngazi ya shule ya sekondari. Niliona itakuwa rahisi kuwaiga wenzao na kufanikiwa ni jambo zuri sana.*


*Nimeona kuwa ni michezo ya Wagogo inayoongozwa na mtaalamu, Dk. Kelmon Mapawa, mtaalamu bingwa wa elimu ya muziki anayestahili kuenziwa na kupongezwa mbona hatuoni kupewa zawadi.*

*Mbona wale wa muziki na kizazi kipya nchini wanaenziwa wakati wa muziki wetu wa Kiafrika hawafanyiwi hivyo?*

*Tunapaswa huduma ziwe kama mashindano na kwa nafasi yangu nampongeza Dk. Kedmon Elisha wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mungu amzidishie uelewa ili na sisi michezo yetu ienee duniani.*

**Joseph yesaya Msindai,**
**Mtunzi wa vitabu,**
**Simu 0712946671,**
**Dar es Salaam.**

# Waziri mulika foleni ya malori Bandari ya Dar




**Na Mwandishi Wetu**

KWA muda sasa madereva wa malori na wadau wa sekta ya usafirishaji, wamekuwa wakilalamikia foleni ndefu katika Bandari ya Dar es Salaam inayotokana na ukaguzi na mzani uliopo bandarini hapo.

Madereva hao wanasema foleni hiyo hutokea wakati uongozi wa bandari unapoyafanyia ukaguzi katika mashine za kukagua mizigo inayotoka au kuingia, ili kubaini kama ina taarifa sahihi ama la.

Ukaguzi ni suala muhimu ili kujiridhisha kuhusu mizigo iliyoko kwenye makontena, lakini wakati mwingine unakuwa ni usumbufu na kwa madereva kwa kutumia muda mwingi.

Ikumbukwe kwamba, baadhi ya mizigo hiyo inakwenda nchi za nje na wasafirishaji wamepewa muda maalum wa kuifikisha kunakohusika.

Kwa maana hiyo, wahusika wa Bandari ya Dar es Salaam, ni vyema wakalichukulia suala hilo kwa uzito ili kuendelea kulinda heshima ya bandari, ambayo imekuwapo miaka mingi.

Kuondoa msongamano wa malori hayo, wakati wa ukaguzi ni suala ambalo liko ndani ya uwezo wa bandari na mamlaka husika na nyingine zinazohusika.

Wadau wanataka litafutwe eneo kubwa la kufanya shughuli hiyo kwani kwa hali ya sasa hata gari likionekana limezidisha mzigo, halina eneo la kuegesha wakati taratibu zingine zikiendelea hali ambayo ndiyo inaleta msongamano huo.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwele, anapaswa kuingilia kati suala hilo badala ya kukaa na kusubiri kila kitu kufanywa na Rais ambaye tunaamini kabisa, hatafurahishwa na habari za foleni hii.

Waziri afahamu kuwa suala la foleni, lina uhusiano mkubwa na tija na uchumi, hivyo wasafirishaji wanapolalamika, lazima ajiulize kwanini na kisha aende akajionee mwenyewe kinacholalamikiwa na kisha kuchukua hatua.

Mbali na msongamano wa malori hayo ya mizigo, inafikia wakati barabara haipitiki kabisa, hata kwa wenye magari binafsi wanaofanya shughuli zao jirani na maeneo hayo.

Kwa mtazamo wangu, ni kwamba hivi sasa ni wakati mwafaka kwa wahusika kuondoa usumbufu, kwani ninaamini hilo linawezekana kwa kuzingatia kwamba muda ni uchumi.

Ikumbukwe, iwapo wateja wa bandari wataona wanatumia muda mwingi kuondoa mizigo yao, wanaweza kuhamia maeneo mengine, hali ambayo haitakuwa kwa afya kwa uchumi nchini.

Inasikitisha kuona, karne hii bado inashindikana kutafuta namna rahisi ya kukagua na kupima mizigo kwa njia, ambayo haitasababisha msongamano kama huo tunaoshuhudia Bandari ya Dar es Salaam.

Madereva wanadai kuwa ukaguzi umekuwa ukiwachelewesha, hali inayosababisha kuwapo foleni ndefu bandarini, hivyo wanapoteza muda mrefu ambao ungeweza kutumika katika shughuli nyingine.

Mmoja wa madereva hao aliyejitambulisha kwa jina la Hamis Dongo, anasema yeye na wenzake wamekuwa wakilazimika kukaa kwa muda mrefu katika foleni kutokana na ukaguzi mbalimbali zinazofanyika bandarini hapo, hivyo anaiomba serikali kuangalia upya namna bora ya kufanya ukaguzi ili kuokoa muda unaopotea.

"Kwa kweli muda tunaopoteza hapa, serikali ingetufikiria, ukiangalia muda unaotumika kukagua gari moja kuanzia kule kwenye mzani ni dakika 30 hadi 50, ukija hapa sasa ndio shida zaidi mara nyingine, tunaambiwa mashine hazisomi...tunaiomba serikali itufikirie," anasema Dongo.

Dereva mwingine anayejitambulisha kwa jina moja la Dafa, anadai mzani uliopo geti namba 12 bandarini hapo ni chanzo cha foleni. Anaishauri serikali kuangalia sehemu ya kuuweka ili kupunguza foleni.

"Huo mzani ni chanzo cha foleni ukizingatia hii barabara inatakiwa kutumika na watu wengi, kuna magari ya abiria hapa na ya watu binafsi, mie ninaona pangetafutwa mahali pengine pa kuwekwa huo mzani badala ya ulipo sasa," anasema Dafa.

Mdau mwingine wa bandari, Abdalah Mfaume, alihoji iwapo itatokea dharura kama ya moto wakati wa msongamano ule, hali itakuwaje kama si madhahara makubwa yanayoweza kutokea kwa watu na mali zao.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Kiwanda cha kutengeneza taa kujengwa kwa bil. 12/-

**Na Beatrice Philemon**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kwa kushirikiana na kampuni ya Everlight Skyzone ya China wanatarajia kujenga kiwanda cha kutengeneza taa za barabarani chenye thamani ya Sh. bilioni 12 za kitanzania.

Lengo kuu la mradi huo ni kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli za kuiingiza Tanzania katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza na Nipashe, msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Kapteni James Mhame, alisema kiwanda hicho kitajengwa jijini Dar es Salaam eneo la Mlalakuwa ambalo ni Makao Makuu ya JKT na kitakuwa na uwezo wa kuajiri watu zaidi ya 50.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho ulianza Aprili mwaka huu na unatarajia kumalizika Agosti mwaka huu.

"Kwa kuanza, kiwanda kitaanza kutengeneza taa za nje (outdoor lights), taa za barabarani, taa za bustani, taa za eneo la maegesho na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha taa 360,000 kwa mwaka," alisema. Alisema wakati wa utengenezaji wa taa kiwanda kitatumia umeme wa maji na umeme wa mwanga wa jua kutengeneza taa hizo.

Kujengwa kwa kiwanda hicho kutaongeza fursa ya ajira kwa Watanzania na kuifanya nchi kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika zenye viwanda vya taa za kisasa (LED) ambayo ni teknolojia mpya barani Afrika.

Vile vile kuwapo kwa kiwanda hicho nchini, kutasaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa taa hizo ambazo kwa sasa zinaagizwa toka nje, na pia kutaifanya Tanzania kuwapo katika orodha ya nchi zenye viwanda vya teknolojia ya kisasa.

Kwa mujibu wa Kapteni Mhame, kupitia mradi huu Watanzania watanufaika na utengenezwaji wa taa hizo kwa kuwa gharama za matumizi ya taa hizo yatakuwa nafuu kwa sababu wakati wa utengenezaji watatumia umeme wa maji na umeme wa mwanga wa jua.

Jengo la maonyesho ya sampuli za taa hizo lipo tayari eneo la Mwenge linalomilikiwa na SUMAJKT na kuna aina 13 za taa ambazo zimeshawasili nchini kwa ajili ya kutangaza na kutafuta masoko na pia kuna aina 100 za taa zipo bandarini kwa ajili ya kuendelea kujitangaza.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea kuona hatua za utekelezaji wa ujenzi wa kiwanda hicho, Makamu wa Rais wa Kampuni ya Everlight Skyzone ya China, Hassan Baalbaki, alisema kiwanda hicho kitatumia teknolojia mpya ambayo haijaenea nchi nyingi za Afrika.



Mfanyabiashara mdogo akitafuta riziki kwa kuuza mito ya kulalia, katika eneo la Ukonga Majumba Sita, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Mimba za utotoni zaitikisa Kagera

**INATOKA UK. 2**

"Wasaidizi wa ndani wa kiume wanaoletwa katika familia zetu wanaweza kuhusika kuharibu watoto wetu. Lakini watoto wetu wanaweza kuhusika kuwapa mimba wafanyakazi wa ndani wa kike. Nashauri jamii kuwa makini na hili na kuwa na tahadhari," alisema.

Edwin Kamaleki, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mabira, alisema kuna changamoto wanapopokea kesi za namna hiyo hasa kutokana na nyingi wanazopokea kutendwa na wanandugu.

"Mara nyingi watu wanakuwa hawajitokezi kutoa ushahidi maana kesi nyingi zinatendwa na wanandugu au wana familia. Kwa hiyo wanakaa na kusuluhishana, hivyo mahakama inakosa ushahidi wa kuendelea na kesi au kumtia hatiani mhusika," alisema.

Mratibu wa Mradi wa World Vision, Bushangaro Nsiima, alitaja kazi ambazo zimefanywa na shirika hilo katika kutokomeza mimba za utotoni katika Wilaya ya Karagwe kuwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wenyeviti wa vitongoji, vijiji, maofisa watendaji wa kata, madiwani na wadau wengine wapato 225.

"Tumeunda pia kamati za ulinzi wa mtoto kwa vijiji 22 ndani ya kata sita ambazo ni Kiruruma, Kamagambo, Rugu, Nyakasimbi, Nyaishozi na Ihembe. Pia tumewajengea uwezo watoto na vijana juu ya stadi za maisha na athari za ndoa za utotoni wapatao 342," alisema.

Katika kufanikisha azma hiyo, alisema pia walifanya mikutano na wazazi na walimu kwa lengo la kuwaelimisha juu ya athari za mimba za utotoni na namna wanavyoweza kukabiliana nazo.

## Operesheni ya Waziri Mpina

**INATOKA UK. 2**

lita 75,000 kwa siku, Machame Dairy Products kinachosindika lita 400 na Bayana Milk lita 100 (Arusha).

Vingine ni Dar es Salaam Zoo Farm Milk Fresh lita 6,000 kwa siku na Gonza Milk lita 700 kwa siku (Dar es Salaam), Mzeituni Business lita 500 kwa siku (Geita), Katavi Dairy Milk Supplier (Katavi) na Nronga Dairy lita 3,000 (Kilimanjaro).

Dk. Mlote alitaja vingine ni Sebadon Milk lita 500 kwa siku (Mbeya), Mazimbu Cheese lita 500 kwa siku (Morogoro), Gema Milk lita 300 kwa siku (Ruvuma), Taishi Milk lita 1,000 kwa siku na Singida Milk lita 500 (Singida), Neema Brands lita 1,000 kwa siku (Tabora) na Bidernan Dairy lita 500 kwa siku (Tanga).

Meneja Mkuu Kampuni ya Galaxy Food & Beverage Ltd wazalishaji wa maziwa ya Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjee, aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa uamuzi wake wa kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa hizo hatua iliyochochea kuanzishwa kwa viwanda vipya. Alisema kabla ya uamuzi huo wa serikali ilikuwa ni vigumu kuanzisha viwanda kutokana na nchi kutawaliwa na bidhaa za maziwa zilizoingizwa nchini kwa njia za panya, huku zikiwa zimekwepa ukaguzi na kutolipa kodi za serikali na kusababisha ushindani usio wa haki kwa wazalishaji wa ndani.

Baadhi ya wabunge wakichangia hotuba ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2019/20 iliyowasilishwa hivi karibuni bungeni mjini Dodoma, walipongeza hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuwalinda wazalishaji maziwa wa ndani ya nchi na kutaka juhudi hizo ziendelezwe ili kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta hiyo.

"Naipongeza wizara kwa kuamua kulinda viwanda vya ndani, wizara na serikali nia yake ni kukuza viwanda vya ndani, nimeona maziwa yetu yanaanza kupata soko kwenye nchi yetu endeleeni hivyo hivyo tuwaunge mkono wazalishaji wa maziwa nendeni muwagundue wengine wanaotaka kuanzisha biashara hii wapeni msaada," alisema Mbunge wa Simanjiro, James Ole Millya.

Akizungumzia mafanikio hayo ya viwanda vipya vya maziwa, Waziri Mpina alisema kamwe serikali haitaogopa lawama katika kulinda rasilimali za nchi, wawekezaji wa ndani, ajira na mapato ya serikali.

Hivyo aliwahakikishia wawekezaji hao na wengine wanaotaka kuwekeza kwenye sekta hiyo kutembea kifua mbele kwa kuwa hakuna mtu yoyote atakayechezea tena soko lao, huku akisisitiza kuwa kutokana na mipango mizuri ya wizara yake, mitamba bora yenye mimba itaendelea kupatikana ili kutosheleza mahitaji ya viwanda nchini. Waziri Mpina alisema tangu wizara hiyo ipoanzisha 'Operesheni Nzagamba', ilikubali lawama kutoka kwa baadhi ya watu na kwamba kama wasingekuwa wavumilivu leo mafanikio ya viwanda hivyo vipya 15 vya maziwa visingekuwapo na kusisitiza kuwa hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na wizara hiyo hazikulenga kumuonea mtu bali zililenga kutengeneza mazingira wezeshi ya biashara hiyo hapa nchini.

# Wawili mbaroni tuhuma kujifanya maofisa usalama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kujitambulisha kuwa ni maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia isiyo halali.

Watu hao ni Mrisho Zabroni (37) na Mgema Patrick (25) ambao walikwenda kwa mmoja wa wafanyabiashara wilayani hapa, Abdallah Moro ambaye ghala lake la kuhifadhia bidhaa lilifungwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema watuhumiwa hao walikamatwa Jumatatu baada ya polisi kuwawekea mtego na kufanikiwa kuwakamata. Alieleza kuwa siku ya tukio watu hao walifika kwenye ghala la mfanyabiashara huyo na kujitambulisha kwake kuwa ni maofisa usalama wa taifa na kumwomba rushwa kiasi cha Sh. milioni tatu, ili waweze kumsaidia kufungua ghala lake. "Moro alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya watu hao waliofika kwake na kujiwasilisha kuwa wao ni maofisa usalama wa taifa na wana uwezo wa kumfungulia ghala ambalo lililokuwa limefungwa na TFDA na kumuomba fedha hizo kama rushwa ili kufanikisha mpango huo," alisema Abwao.

Abwao amewataka wananchi na wafanyabiashara wote kuwa makini na watu wanafika kwenye biashara zao hasa maofisa ukaguzi wanapofungiwa maghala yao na kujitambulisha kwao kuwa ni maofisa usalama wa taifa, na kwamba wasisite kutoa taarifa ili wachukulie hatua za kisheria.



Sheikh wa Mkoa wa Kigoma, Hasani Kiburwa, akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye sikukuu ya Eid El Fitr, juzi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

## TFDA yaagiza wasindikaji

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MAMLAKA ya Chakula na Dawa (TFDA) imewataka wasindikaji wadogo wa chakula mkoani Mara kuzingatia taratibu na kanuni za usafi katika eneo la usindikaji, ili kuzuia vimelea vya magonjwa kuingia kwenye bidhaa wanazozalisha kwa lengo la kulinda afya ya mlaji.

Akitoa agizo hilo mjini Musoma kwenye mafunzo ya wajasiriamali wadogo wanaosindika vyakula, Kaimu Meneja TFDA Kanda ya Ziwa Mashariki, Nuru Mwasulama, alisema ni vyema wazalishaji wa vyakula vya aina hiyo kufikisha elimu waliyopewa kwa wafanyakazi wao wanaosaidia kutengeneza vyakula hivyo.

"Wafanyakazi wanatakiwa kupimwa afya na ofisa afya aliyesajiliwa mara wanapoajiriwa na kila baada ya miezi sita, magonjwa kama kifua kikuu, minyoo, homa ya matumbo, kuhara na kuhara damu yanatakiwa kuchunguzwa na kutolewa majibu ya kitabibu na hizo taarifa zote za uchunguzi wa afya za wafanyakazi zitunzwe," Nuru aliagiza.

Alisema iwapo mfanyakazi atagundulika kuwa na maradhi yaliyotajwa hataruhusiwa kufanya kazi kiwandani mpaka atakapopona.

Kadhalika alisema kiwanda kinatakiwa kuwa na sehemu maalumu zenye nafasi za kutosha kubadilisha nguo, maliwato na bafu ikiwamo sehemu ya kunawa mikono, na kwamba vyote vinatakiwa kukidhi mahitaji ya jinsia zote.

Dokta Bahati Midenge, muwasilishaji wa mada ya kanuni bora za usindikaji katika mafunzo hayo, alisema ili kukidhi viwango vya ubora na usalama wakati wote bidhaa zinapotengenezwa eneo la uzalishaji linatakiwa kuwa mbali na vyanzo vya uchafuzi wa mazingira kama vile harufu mbaya, moshi, vumbi jingi, jalala, mabanda ya wanyama na mifereji ya maji machafu iliyo wazi.

"Malighafi na bidhaa zilizosindikwa zinatakiwa kuhifadhiwa katika hali ambayo itazuia uchafuzi au uzalishwaji wa wadudu waharibifu au wale wanaotengeneza sumu, hivyo kuzuia malighafi, bidhaa au vifungashio kupoteza ubora. Kuwe na sehemu zilizotengwa kuhifadhia malighafi, bidhaa zilizozalishwa, vipuri na mabaki ya uzalishaji," alisema.

# Mdau ajitolea kutangaza vivutio vya utalii Tanzania ughaibuni

**Na Beatrice Philemon**

VIVUTIO vya utalii vilivyopo Tanzania vitaanza kujulikana Ukraine baada ya mshindi wa Shindano la Urembo la Dunia 2018 linalohusisha wanahabari kutoka Ukraine kuahidi kuitangaza Tanzania kama kivutio bora cha utalii ulimwenguni.

Hatua hiyo itasaidia kuvutia watalii wengi kutembelea Tanzania.

Hayo yalisemwa na mshindi wa shindano hilo, linalohusisha wanahabari, Nina Yeutusheko, aliyekuwa nchini kwa wiki mbili kujionea vivutio vya utalii vilivyopo nchini, ili aweze kusaidia kutangaza vivutio hivyo Ukraine na nchi zingine ulimwenguni.

Alisema akiwa Ukraine atatumia mfuko wake wa (Nina Foundation) na vyombo vya habari na mtandao wake wa kijamii.

"Ukraine ipo mbali sana na asilimia kubwa ya wananchi wake hawajui aina ya vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania, ni vizuri wakala wa kusafirisha watalii kuanzisha baadhi ya miradi Ukraine ambayo itawaelisha wananchi kuhusu Tanzania, aina ya vivutio vya utalii vilivyopo, jinsi gani wanaweza kufika nchini, usalama wa watalii wakiwa nchini na masuala mengine.

Alisema kama wananchi watajua kuwa Tanzania ni nchi nzuri na salama, itakuwa rahisi kwao kuja katika makundi kutembelea vivutio vya utalii nchini.

"Nimefurahi sana kutembelea mbuga za wanyama, Tanzania ni nchi nzuri sana yenye kuvutia, sijawahi kuona mazingira mazuri kama hapa, nimefurahi kuona jinsi wanavyohifadhi mbuga za wanyama, jinsi miti na majani vinavyohifadhiwa tofauti na nchini kwetu, ambapo watu wanakata sana miti kwa ajili ya shughuli zao binafsi na pia sijaona takataka yoyote mbugani," alisema.

Vile vile alisifia ukarimu wa Watanzania, akisema ni wenye upendo na furaha kwa sababu walimpokea vizuri sana na walikuwa kama ndugu kwake.

Akaeleza kuwa amefurahi sana na atarudi tena Novemba mwaka huu kwa ajili ya kuutangaza zaidi Mlima Kilimanjaro. Vile vile akiwa Zanzibar, amesifia fukwe za Zanzibar kuwa ni nzuri sana.

Pia aliishuruku Kampuni ya kitanzania ya Miss World Tourism na Bodi ya Utalii Tanzania kwa kumpatia nafasi ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania.

"Sasa hivi nafahamu naweza kusema nini kuhusu Tanzania nchini Ukraine na nchi zingine ulimwenguni kwa sababu nimetembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Ngorongoro, Zanzibar, Dodoma na kutembelea Bunge na kukutana na wabunge," alisema

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii, (TTB), Devota Mdachi, alimshukuru Nina kwa kutembelea Tanzania na kujionea vivutio vya utalii vilivyopo.

Anasema akiwa nchini Nina alitembelea vivutio vya utalii ikiwamo kutembelea Bunge na alipokelewa kwa kishindo na atashirikiana na TTB kutangaza vivutio vya utalii Ukraine na nchi zingine ulimwenguni.

"Bodi ya utalii imekuwa ikijaribu jinsi ya kuingia kwenye soko la utalii la Ukraine kwa muda mrefu Nina atashirikiana na vyombo vya habari vya Ukraine, mfuko wake wa Nina na mtandao wake wa kijamii kutangaza vivutio vyetu vya kitalii Ukraine," alisema.

Anasema Nina atasaidia Bodi ya Utalii kufungua milango zaidi kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea Tanzania.

"Kwa kuanzia, tunatarajia angalau kupokea watalii 10,000 kutoka Ukraine kwa mwaka 2020 kwa sababu atashirikiana na vyombo vya habari, mfuko wake wa Nina Foundation na mitandao mingine ya kijamii kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania," alisema Mdachi.

# Mradi wanufaisha vijana kwa kujiajiri

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

ZAIDI ya vijana 40 mjini Musoma mkoani Mara, wamenufaika na mradi unaotoa mafunzo wezeshi kupitia sekta ya elimu na ubunifu, hivyo kujiondoa katika dhana ya kuajiriwa.

Mradi huo mpya unaoitwa Bsmarty Academy ulizinduliwa mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu Duniani yalioanza kusherehekewa kwa mara ya kwanza nchini kuanzia Aprili 15 hadi 21 kila mwaka.

Wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi wa mradi huo, Boniphace Ndengo, alisema ili kutoa fursa kwa vijana nchini mradi utawajengea uwezo wa kitaaluma na ubunifu kwa kufanikisha ndoto na njozi zao katika taaluma, uongozi na ujasiriamali.

Alisema kila mwaka zaidi ya vijana milioni moja huingia katika soko la ajira baada ya kuhitimu masomo yao wakiwa ni tegemezi kifikra na kiutendaji, pia wakiwa na matarajio ya kuajiriwa.

"Wachache wanaojitosa katika kujiajiri hukumbana na vikwazo vya kutosha ikiwamo changamoto za mitaji, uwezo mdogo wa ubunifu, masoko yasio ya uhakika, na urasimu katika mfumo wa tozo lukuki za kodi," alisema Ndengo.

Alisema mradi huo umeshatoa takribani milioni 30 kusapoti vijana hao waliojifunza ujasiriamali na ubunifu wa utengenezaji wa sabuni, ufugaji kuku, bidhaa za kusindikwa, mapambo, uundaji wa vinanda, power bank na nyingine.

"Tunapoadhimisha siku hii ya ubunifu duniani tumekusudia katika kipindi cha miaka mitano (2019/2024) kupitia mradi huu kuwa tumepunguza changamoto hizi angalau kwa asilimia 50," alieleza.

Ofisa elimu mkoani Mara, Emanuel Kisongo, alishukuru uongozi wa mradi huo na kutoa wito kwa walimu wa shule za sekondari na msingi kufufua klabu za masomo, ili kupunguza tatizo la kufeli hasa somo la Hisabati.

# 'Aibu Dar kuwa na kipindupindu'

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo, amesema ni jambo la aibu kuona jiji kubwa kama la Dar es Salaam ambalo linakua kwa haraka kiuchumi linakumbwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Kauli hiyo aliitoa jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) pamoja na kamati ya maendeleo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema kuwa hivi karibuni wizara ilituma wataalamu kwenda kupima ubora wa maji katika maeneo nane na majibu yakaja asilimia 99 ya wanaotumia maji sio kutoka dawasa, kwa maana hiyo inaonyesha kwamba wananchi wakiunganishiwa katika mtandao wa maji ya Dawasa kipindupindu hakitatokea tena.

"Katika sampuli nane zilizopimwa, asilimia 99 katika maji hayo sio mtandao wa Dawasa watu wamejiunganishia wenyewe kwa hiyo watu hao wakiunganishwa na Dawasa itakuwa njia ya kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu kwa asilimia 90," alisema na kuongeza:

"Jiji ambalo lina maskini wachache nchi nzima chini ya asilimia 5, jiji ambalo kipato chake ni kikubwa, jiji ambalo serikali imewekeza sana katika miundombinu ni lazima jambo hili dogo la kipindupindu liishe."

Kutoka na hali hiyo, Prof. Mkumbo alitoa maagaizo matatu kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemaje, kujenga vituo vya kuchota maji ya Dawasa (vioski) ili wananchi wapate mfumo rasmi wa serikali kupata huduma ya majisafi katika maeneo ambayo yameathirika ikiwamo Vingunguti.

Pili, lazima Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu wakague na kusajili visima vyote jijini Dar es Salaam vinavyomilikiwa na watu binafsi.

"Bodi wameshaanza hii kazi... maana katika sampo ya visima nane, visima saba vyote vya watu binafsi kwa maana hiyo visima hivi lazima vikaguliwe na lazima visajiliwe ili tuvijue na kufahamu hawa wananchi wanatumia maji ya aina gani," alisema Prof. Mkumbo.

Aliongeza kuwa katika visima hivyo nane vilivyofanyiwa uchunguzi, Dawasa lazima wakaweke dawa ya kutibu maji kwa kuwa jukumu la serikali ni kulinda uhai wa watu wake.

Pia alisema ni lazima Dawasa iwe na utaratibu wa kujenga uhusiano mzuri na wananchi wote ambao wanatumia maji ambayo sio ya mamlaka hiyo ili kutoa elimu kwamba kumiliki kisima kwa kufuata kanuni na taratibu.

"Hivi karibuni Waziri (Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa) alitangaza kuruhusu watu kumiliki visima kwa matumizi ya majumbani bila kutotozwa tozo yoyote... kwa maana hiyo wananchi wengi wataongezeka kumiliki visima vya maji majumbani kwao jambo ambalo ni jema muhimu, ni kufuta taratibu na sheria," alisema.

Prof. Mkumbo alitoa wito kwa wananchi kuendelea kuzingatia suala la usafi wa mazingira kwa sababu ugonjwa wa kipindupindu ni matokeo ya kutokuwa na usafi katika maeneo yanayowazunguka.

Alisema kuwa serikali haiwezi kumaliza kipindupindu kama wananchi hawatakuwa mstari wa mbele kuzingatia usafi na kula vyakula katika mazingira ya usafi kwani haipendezi na sio sawa Jiji la Dar es Salaam kukumbwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Alisema jambo la tatu, kwa Dawasa ni suala la usalama wa maji kutokana na ukweli kwamba katika Jiji la Dar es Salaam ni miongoni mwa majiji matatu Afrika yanayokuwa kwa kasi sana na miongoni kwa majiji tisa duniani yanayokuwa kwa kasi kwa maana idadi ya watu inaongezeka kwa kasi.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba John Kabudi (katikati), akishauriana jambo na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stagomena Tax, jijini Dar es Salaam juzi, kabla ya kuanza kikao cha awali cha mashauriano kuhusu mkutano wa SADC unaotarajiwa kufanyika hapa nchini mwezi Agosti 2019. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Faraji Mnyepe. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Viongozi vyama vya siasa wapewa neno

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

VIONGOZI wa vyama vya siasa mkoani Singida, wameshauriwa kutochanganya dini pamoja na siasa kwenye shughuli za maendeleo, kwa kuwa hali hiyo inaweza kuchangia kuleta mfarakano katika jamii.

Msimamizi wa kitengo cha elimu cha Taasisi ya Islamic Foundation Mkoa wa Singida, Yakhini Saidi Mkokoo, ndiye aliyetoa ushauri huo alipokuwa akitoa mawaidha kwenye Baraza la Eid Wilaya ya Singida Vijijini kwenye viwanja ya msikiti uliopo katika Mji Mdogo wa Ilongero.

Mkokoo ambaye pia ni mwalimu wa dini ya kiislamu, alisisitiza kwamba iwapo viongozi wa siasa wataanza kuwatenga watu kwa sababu ya siasa kwenye uchangiaji wa shughuli za maendeleo, upo uwezekano mkubwa kuzuka kwa mtafaruku katika jamii.

"Lakini inapofika mahali viongozi wa vyama vya siasa wanaanza kuwatenga watu kwa sababu ya siasa, hali hiyo italeta mtafaruku katika jamii, lakini kama siasa itashika nafasi yake, dini ikawaunga watu wakawa kitu kimoja na siasa ikawaunga watu kwa maneno mazuri, kila jambo litaenda vizuri," alifafanua.

Mkokoo ambaye pia Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Answary Muslimu Yuoth Centre, aliwatahadharisha viongozi wa kisiasa kutotumia nafasi zao kuwagawa makundi au matabaka baadhi ya watu katika vyama vya siasa.

"Kwa ujumla dini ya kiislamu ni dini ambayo haijapinga siasa, bali ni dini pia ina siasa ndani yake," alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Katibu wa Bakwata Mkoa wa Singida, Alhaji Buruhani Mlau, alisisitiza kwamba kazi kubwa ya viongozi wa madhehebu ya dini ni kuunganisha taasisi za dini kuwa kitu kimoja.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula (wa tatu kulia) na mdau wa maendeleo Charles Mnyalu (wa pili kulia), wakigawa chakula kwa watoto yatima wa Mji Mdogo wa Mirerani, kilichoandaliwa na Mnyalu kwenye maadhimisho ya sikukuu ya Eid El Fitri juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Nchi 45 kushiriki Karibu Kili Fair leo

**Novatus Makunga,** ARUSHA

ZAIDI ya nchi 45 zinatarajiwa kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ya utalii yanayofahamika kama Karibu-Kili Fair, yanayofunguliwa na Waziri wa

Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla leo, jijini Arusha.

Mkurugenzi wa maonyesho ya utalii ya Karibu-Kili, Dominic Shoo, alisema zaidi ya mawakala na wadau wa utalii 600, kutoka nchi hizo pamoja na nchini watashiriki katika maonyesho hayo ya siku tatu.

"Hawa ni mawakala wenye ushawishi mkubwa sana katika sekta ya utalii na kwa ujumla tunawaita wanunuzi kwa maana ndiyo wenye uwezo wa kuuza vivutio vya utalii, ndani ya nchi wanazotoka, kwa ujumla maonyesho haya ni muhimu sana kwa taifa letu," alifafanua.

Alisema licha ya kushiriki katika maonyesho hayo, pia watapata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali ili kujionea vivutio vilivyopo, kabla ya kwenda kuviuza kwa kasi kubwa katika nchi wanazotoka.

Shoo alisema katika maonyesho ya mwaka huu, kuna matarajio ya kuona huduma mpya katika utalii ambazo ni ngeni kwa watu wengi.

"Baada ya maonyesho hayo tunaamini vivutio mbalimbali vya utalii vya Tanzania vitakuwa vimetangazwa vyema na hivyo tutarajie taifa kupokea idadi kubwa ya watalii," aliongeza.

Shoo alisema maonyesho ya mwaka huu yameongezeka umuhimu wake kutokana na kushirikisha nchi kumi, ambazo zinaongoza kwa kuwa chanzo cha watalii wanaotembelea bara la Afrika, ikiwamo Tanzania ambazo baadhi alizitaja kuwa ni pamoja na Ujerumani, Marekani, Uingereza na Australia.

Hata hivyo, alisema pia katika maonyesho hayo kuna ushiriki wa nchi ambazo ni masoko mapya alizozitaja kuwa ni Italia, Ubelgiji na Urusi ambao wamefungua kwa ajili ya Tanzania.

Shoo alisema kutakuwa na semina kuhusu utalii wa dunia ambazo zitaendeshwa na wabobezi zaidi ya 30 katika utalii kwa lengo la kufundisha mbinu za kusimamia, kuhudumia na kuendeleza utalii wa ufanisi zaidi.

"Hizi semina haziaangalii utalii wa Tanzania bali wa dunia nzima kwa kuwa hawa ni wanunuzi wa kimataifa wa utalii wenye uzoefu mkubwa ambao unajumuisha kila pembe ya dunia, mafanikio na changamoto zake, lakini pia mbinu na njia ya kujinasua," alisema.

Shoo akizungumzia maonyesho ya mwaka huu, alisema yamekuwa mwamko mkubwa tofauti na kipindi cha miaka mitano iliyopita, wakati yanaanza na

miaka miwili baada ya wadau wote wa utalii kuungana na kuwa na maonyesho ya pamoja kwa kubadilishana katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na maonyesho hayo ni makubwa zaidi ya utalii katika eneo la Afrika ya Mashariki, yakifanyika kila mwezi Juni ya kila mwaka.

# Mifuko ya plastiki yazagaa Sinya

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

LICHA ya katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki, maeneo mengi ya Jumuiya ya Enduiment (EWMA), katika Kata ya Sinya, wilayani Longido, imeonekana kukithiri kwa mifuko hiyo na kuleta athari kwa binadamu, wanyamapori na wafugwao pamoja na viumbe hai.

Shirika la Maendeleo ya Jamii OIKOS East Afrika limewezesha utekelezaji wa usafi katika soko la Kata ya Sinya, Tarafa ya Enduiment chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumza jana na gazeti hili, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Shirika hilo, Zacharia Laizer, alisema lengo la kufanya usafi katika eneo hilo ni kuunga mkono juhudi zinazotekelezwa na serikali kuhusu uhifadhi wa mazingira, kwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. "Kwanza tunaunga mkono serikali hii, lakini tumeona serikali imekataza matumizi ya mifuko hiyo, lakini maeneo ya jumuiya bado ipo inazagaa, hivyo tumelazimika kufanya usafi kwa kushirikiana na klabu ya mazingira ya Shule ya Msingi Sinya," alidai.

Alisema kuwa kata hiyo ipo katika hifadhi ya wanyamapori ndani ya Jumuiya ya Enduiment (EWMA) na ni eneo lenye watalii wengi kwasababu hupenda kufika kwa ajili ya kuona wanyamapori mbalimbali na utamaduni wa Kimaasai.

"Ukienda katika hifadhi zingine, utakuta vyombo maalum vya kutupia taka, lakini katika hifadhi hii ya EWMA hakuna na ukiangalia watu wanatupa taka popote, mazingira yanakua si rafiki kwa viumbe hai na hata watalii hawependi mazingira machafu," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo wamelazimika kutoa elimu katika shule mbalimbali ndani ya tarafa hiyo kuhusu uhifadhi wa mazingira, wakiamini wanafunzi hao wakirejea nyumbani baada ya masomo, wataenda kuwa mabalozi wazuri kwa wazazi na jamii.

"Shirika hili lina programu inayoitwa "Citizen Science Education" inalenga uhifadhi wa mazingira na tunafundisha watoto wa shule, tumeshatoa elimu kwa baadhi ya shule na tunaendelea," alifafanua.

Alisema mifuko ya rambo inaathari kwa maisha ya wanyamapori, wafugwao na binadamu, kwa kuwa wanyama wakila mifuko hiyo wanakufa na tarafa hiyo inawafugaji wengi, lakini wanaishi mazingira hayo na wanyamapori.

Alieleza kuwa, jumuiya hiyo ikipokea kauli ya serikali na baadhi ya mashirika ya uhifadhi wa mazingira kupitia idara ya utalii watapata fedha za kutosha, kwa kuwa watalii wengi watavutiwa kutembelea uhifadhi wa jumuiya hiyo.

# World Vision yatoa msaada wa vitimwendo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

SHIRIKA la World Vision Tanzania (WVT), limewanasua watoto wenye ulemavu wa aina tofauti kuondokana na adha ya kushindwa kwenda shule kwa kutambaa na kupita kwenye maji na miiba, baada ya kuwapatia vitimwendo.

Hayo yalisemwa jana kwenye ofisi za shirika hilo, Magugu wilayani Babati mkoani Manyara na Meneja wa Kitengo cha Maafa anayeshughulikia mradi wa utoaji viti kwa watoto wenye ulemavu, kutoka World Vision, Victor Katambala, wakati wa kuwapima watoto kulingana na aina ya magurudumu ya vitimwendo yenye meza.

Alisema msaada huo wa vitimwendo 25 umegeuza mawazo na mitazamo ya wazazi na walezi wa watoto hao wenye ulemavu, ambao walikuwa wakifichwa kwa kuhofia kuwatoa nje, ili waishi maisha sawa na watoto wengine.

"Tuna mpango wa kutoa viti 164 kwenye Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro na Manyara na kabla ya kutoa viti tunatoa semina kwa wakunga wa afya vijijini ili wasaidie kuufanya mradi kuwa endelevu," alisema.

Aidha, alisema viti hivyo wamepewa World Vision Tanzania kama msaada kutoka World Vision Australia na wao wamevitoa na kuviunganisha kwa ushirikiano na CCBRT Moshi, ili kusaidia wazazi walezi wa watoto hao waweze kufanya shughuli za kiuchumi kwa sasa, kwa kuwa watoto wataweza kutembea wenyewe.

Katambala alisema wameshafanya semina kwa wahudumu wa afya vijiji 80 wilayani Same mkoani Kilimanjaro, Arusha na Babati na baadaye Karatu na muda waliofanya kazi na wananchi wa maeneo hayo wamegundua watoto wengi wana ulemavu uliosababisha wakose elimu na mahitaji mengine. Alisema watoto wenye ulemavu baadhi yao wameshindwa kutembea, kwenda shule na kucheza na wenzao, huku wazazi wao wakishindwa kutekeleza majukumu ya maendeleo kutokana na kulazimika kuwa nao karibu.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi World Vision Magugu, Majidi Mfinanga, alisema wamekuwa wakifanya kazi na wahudumu wa afya vijijini, ili kusaidia kuwapata watoto wenye ulemavu.

Alisema wamegawa vitimwendo kwa watoto 25 na baada ya hao, watoto wenye uhitaji wamezidi kuongezeka.

"Hali hii inaonyesha kuwa wananchi wamekuwa wakiwaficha ndani watoto wenye ulemavu, hivyo tunawaomba wawaone watoto wenye ulemavu kama watoto wengine ili wapate huduma stahiki," alisema.

Alisema watoto wenye ulemavu wana haki ya msingi ya kwenda shule, kutembea au kucheza kama watoto wengine na lengo la World Vision Tanzania ni kuona mtoto anapata huduma na haki zake za msingi. Alitaja baadhi ya haki zao ni kucheza, kutembea na wenzake kwa hiyo wanapopata viti kama hivyo vinawawezesha kuchangamana na watoto wenzao, sababu mtoto akikosa kucheza na wenzake ana athirika kisaikolojia na kuja kuwa mzigo kwa familia yake.

Naye Mkazi wa Magugu, Shaban Abdallah Majimoto, baba mzazi wa Fatuma (14), anayeishi na ulemavu, aliishukuru WVT kwa kuona changamoto zinazowakabili watoto wenye ulemavu.





# Kibarua kizito madiwani waliopita bila kupingwa

**Na Paul William,** MOSHI

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, amewapa kibarua kizito, madiwani wateule waliopita bila kupingwa Deogratius Mushi wa Kibosho Magharibi na Bertin Mkami wa Kata ya Uru, Shimbwe, kuhakikisha wanalirejesha Jimbo la Moshi Vijijini mikononi mwa CCM.

Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa sasa ni Athony Komu ambaye aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Fedha ni Katibu Utawala Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mabihya aliwapa kibarua hicho jana, wakati wa kuwashukuru wananchi wa kata hizo kwa kitendo chao cha kuwaamini wagombea hao na kutosimamisha wagombea wengine na kusababisha madiwani hao kupita bila kupingwa.

Juzi, madiwani hao walikabidhiwa hati maalum za kupita bila kupingwa katika uchaguzi wa marudio ya udiwani na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Moshi, Castory Msigala.

"Nendeni mkawatumikie wananchi wenu kwa kutatua changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo mlikwama kuiitatua mkiwa vyama vya upinzani, lakini jambo kubwa lililo mbele yenu na tunataka mliishi hivi sasa ni kwamba ni lazima mtusaidie kulikomboa jimbo," alisema.

Mabihya alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kuwashukuru wananchi wa kata hizo kwa kitendo chao cha kuwaamini wagombea hao na kutosimamisha wagombea wengine na kusababisha madiwani hao kupita bila kupingwa.

Alisema lengo la CCM ni kuwatumikia wananchi bila kujali itikadi za vyama vyao na kuwataka madiwani hao wateule kuwaunganisha wananchi wa kata hizo mbili katika kusukuma mbele maendeleo ya kata hizo.

Katibu huyo alisema kuwa, madiwani hao wakifanya majukumu yao kwa ufanisi mkubwa yatapelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu, kuwa mwepesi katika kata hizo mbili.

"Kitendo cha kupita bila kupingwa ni dhahiri kuwa wananchi wanawaamini mnaweza kuwatumikia itekelezeni imani hiyo kwa vitendo, ili tukifika katika chaguzi za serikali za mitaa tuwe kama tunamsukuma mlevi," alisema Mabihya.

Kwa upande wake, diwani huyo mteule wa Kata ya Uru Shimbwe, Bertin Mkami, alidai awali alikuwa katika chama cha Chadema kisicho na Ilani na badala yake ni chama cha migogoro hali ambayo ilikuwa ikimkwamisha kuwaletea maendeleo wananchi na kuwaahidi kushirikiana nao katika maendeleo.

Naye Diwani Mteule wa kata ya Kibosho Magharibi, Deogratius Mushi, aliahidi kuhakikisha anawaunganisha wanachama na CCM pamoja na wananchi wa kata hiyo kuwa wamoja katika kusukuma gurudumu la maendeleo bila kuangalia itikadi za vyama vyao.



Mkazi wa Jiji akipita jirani na shimo kubwa lililopo barabarani eneo la Mwananyamala Sokoni, jijini Dar es Salaam jana, ambalo linasababisha usumbufu na uharibifu kwa vyombo vya moto. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Hospitali Hai yamkosha RC Mghwira

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WATAALAMU wa Sekta ya Afya katika Wilaya ya Hai, ambao wanafanya kazi ya kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotumia bima ya afya 'wamemkosha' Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kutokana na kufanya vizuri zaidi kwenye makusanyo ya na matumizi ya fedha, kati ya wilaya zake sita.

Dk. Mghwira amesema kuwa serikali inaridhishwa na makusanyo na matumizi ya fedha za bima ya afya ya Hospitali ya Wilaya ya Hai.

Katika taarifa yake, mkuu huyo wa mkoa amesisitiza kuwa hospitali nyingine za wilaya katika Mkoa wa Kilimanjaro zinaelekezwa kuiga kinachofanywa na Hospitali ya Wilaya ya Hai.

"Kama kuna watu wanifurahisha na kwa kweli niseme wazi kwamba naridhishwa sana na matumizi ya fedha yanayofanywa na wataalamu wa Hospitali ya Wilaya ya Hai. Wengine sijui tunakwama wapi? Alihoji na kusisitiza:

"Matarajio ya wananchi mara baada ya kujiunga na bima ya afya ni kupata huduma bora za afya bila usumbufu, huku wakiwa na uhakika wa kupata dawa kwa makundi yote ikihusishwa wale wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya Ngazi ya Jamii (CHF) na Bima ya Afya iliyoboreshwa (ICHF)."

Dk. Mghwira alisema hospitali hiyo imetumia fedha ya bima ya afya kujenga vyumba vinne vya kisasa ambavyo vitatumika kwa matumizi mbalimbali hospitalini hapo.

Pia ameeleza kuridhishwa na thamani ya fedha zilizotumika kujenga wodi ambazo zitasaidia kuboresha huduma ya afya pamoja na kuondoa msongamano wa wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hiyo.

Kutokana na umakini huo wa wataalamu wa wilaya ya Hai, Mghwira amezitaka halmashauri zote za Mkoa wa Kilimanjaro kuwa na tabia za kutumia fedha zinazopatikana kuboresha huduma za kijamii, badala ya kuendelea kusubiri utekelezaji wa miradi kutoka serikalini.

Kwa kuwa bima ya afya, kwa sasa ndiyo suluhisho la uhakika wa matibabu, wananchi wametakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya, ili kuwa na uhakika wa kupata matibabu wanapofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

"Ni muhimu kwa wananchi kuwa na bima ya afya ili waweze kuwa na uhakika wa kupata matibabu ikiwamo dawa bila ya kikwazo cha fedha," alisisitiza Mghwira.

# Wagonjwa moyo kusaidiwa Julai

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

AWAMU ya pili ya mpango wa kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum wakiwamo wagonjwa wa moyo ambao unatekelezwa na Taasisi ya Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Martin Shao, unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai, mwaka huu.

Akizungumza jana na wadau wanaojitolea kufadhili mpango huo, Dk. Shao, alisema taasisi hiyo itaendelea na mpango huo wa kupima afya na kufanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kwa watoto wa shule za msingi hasa waliopo pembezoni na wale ambao hawawezi kuzifikia gharama za matibabu.

"Tunakusudia kuendelea tena na mpango wa uchunguzi wa afya kwa wale wasioweza kumudu gharama za kufikia matibabu na kufanyiwa uchunguzi. Mpango huu unatekelezwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha," alisema.

Ili kufikia malengo ya mpango huo, Askofu Shao alisema uwekezaji kwa wenye mahitaji maalum ni lazima, kwa kuwa ni huduma yenye faida au baraka kwa mtendaji na watendewa na kwamba uwekezaji huo ndiyo benki pekee isiyofilisika kwa sasa.

"Tuwekeze katika benki hii kwa kutenda mema kwa sababu benki ya Mungu haifilisiki hasa kwa wanaowekeza kwa watu wenye mahitaji maalum ambayo ni huduma ya faida/baraka kwa mtendaji na mtendewa. Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana (Mungu) naye atamlipa kwa tendo lake jema," alisema.

Katika taarifa yake kwa wadau hao, Dk. Shao ambaye ni mwasisi wa taasisi hiyo ameeleza kuwa mpango huo unalenga kuwatafakarisha kuhusu wito wa kumfanya mwanadamu mwenzao aishi kwa furaha, amani, upendo na akijenga tumaini lenye uzima.

Kwa mujibu wa Askofu Shao, malengo makuu matatu yaliyomsukuma kuanzisha taasisi hiyo ni kusaidia wasiojiweza kufikia gharama za matibabu ya magonjwa ya moyo ikiwa ni pamoja na watoto wanaozaliwa na magonjwa ya moyo.

Malengo mengine ni kusaidia yatima na wahitaji kulipia gharama za huduma za afya na matibabu kwa kushirikiana na hospitali au vituo vinavyotoa huduma ya afya na kusaidia yatima na wahitaji kufikia malengo yao ya kielimu kwa kutoa udhamini kwa wanafunzi kuwawezesha kulipa gharama mbalimbali za masomo.

Pamoja na mambo mengine, taasisi hiyo inalenga kujikita zaidi kuona yaliyofanyika, changamoto zilizopo na kuchangia kwa mawazo kuhusu nini kifanyike katika kutunza malengo hayo makuu matatu ya taasisi hiyo.

Jumla ya gharama zilizotumika katika matibabu kwa wahitaji hao kati ya mwaka 2016 hadi 2018 ni Sh. 10,433,800.

Mpaka kufikia sasa, wanafunzi zaidi ya 3,035 wa shule za msingi katika wilaya za Moshi, Siha na Hai, mkoani Kilimanjaro ambao ni wanufaika wakuu wa huduma ya uchunguzi wa magonjwa ya moyo na afya kwa ujumla wake, wameiweka Taasisi ya Askofu Martin Fuatael Shao (BMFSF), katika orodha ya taasisi zinazoongoza kwa huruma katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini.



UPIMAJI KIDIGITALI WALETA MAISHA MAPYA UTAJIRI ARDHI MOROGORO

Ukurasa 16





Ndege ya wanawake pekee

Ukurasa 15

# BUFE

Ijumaa Juni 7, 2019
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## BIDHAA SAMAKI

# Tafiri waingia ubia na wadau kupigania dagaa, migebuka wa Ziwa Tanganyika

Ukurasa 14

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

Na Renatha Msungu, aliyekuwa Kigoma

## BIDHAA SAMAKI...

# Tafiri waingia ubia na wadau dagaa, migebuka wa Ziwa Tan

- Ukame mkuu ni ufadhili wa utafiti
- Mara ya mwisho imepita miaka 24

ILI kunusuru rasilimali kuu ya ziwani, mtoni na baharini ni maji bora na samaki, kazi inayohitaji kuwapo rasilimali ya ujuzi na vifaa au mahitaji mengineyo.

Si samaki wote wanaofanana kila mahali. Katika Ziwa Tanganyika lililopo mkoani Kigoma, samaki wakuu wanaopatikana huko ni migebuka na sangara.

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, kituo cha Kigoma (Tafiri-Kigoma), inalalamika kuwa upungufu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanyia utafiti katika Ziwa Tanganyika, ni mtihani mkubwa unaoikabili.

Mbali na Kigoma, Tafiri inahudumia vituo vingine vya utafiti Ziwa Victoria (Nyegezi, Mwanza), Ziwa Nyasa (Kyela) na Kunduchi (Dar es Salaam).

Mkoani Kigoma, utafiti unaangalia wingi wa samaki katika Ziwa Tanganyika, ubora wa maji, hali ya uvuvi na kuishauri serikali cha kufanya na kisha inaitaarifu jamii walichokibaini.

Changamoto hiyo imeonekana kikwazo kikubwa katika taasisi hiyo na kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi, tofauti na matarajio ya kituo, ikiwamo watafiti wenyewe ambao wanakwazwa na adha ya ukosefu wa vifaa kituoni.

Miongoni mwa yanayosisitiziwa, ni kwamba wanaangalia mazingira ya samaki wanakoishi na ubora wa viumbe vingine wanaotegemeana katika mfumo wa chakula.

Hapo kinachofanywa ni ukaguzi wa chakula cha samaki, vimelea vya viroboto majini na virutubisho maji (mbolea) kama vile Naitrojeni na Fosiforasi na bakteria, katika athari zinazochangia kupungua samaki ziwani.

**Mtafiti Tafiri**

Mtafiti Mwandamizi wa Tafiri Kigoma, Athanasio Mbonde, analalamika changamoto kuu inayokwamisha ufanisi ni ukosefu wa vifaa vya kisasa.

Mbonde anatoa mfano, bado wanatumia vifaa vya kizamani katika kuangalia chakula cha samaki majini, ambavyo vinachangia kuchelewesha ufanisi wa kazi yao.

Pia, ofisa huyo mtafiti anasema wako katika malengo ya

kukifanya kituo hicho cha Tafiri kuwa cha kimataifa na wakawa na maabara ya kimataifa.

Inaelezwa kuwa Ziwa Tanganyika, lililomo katika bonde la ufa wa Afrika Mashariki, lina uwezekano mkubwa wa mazingira yake kuchafuliwa na kusababisha madhara kwa viumbe wanaoishi.

**Mkuu Tafiri**

Mkurugenzi wa Tafiri, Dk. Ismael Kimirei, anasisitiza umuhimu wa utafiti katika uvuvi, kwamba ufanisi wake utaleta matokeo chanya yanayoisaidia jamii kwa usalama wa chakula na serikali kuingiza mapato ya biashara zitokanazo na mazao ya uvuvi ziwani.

Ombi la Dk. Kimirei kwa serikali, ni kwamba iwatengee fedha za utafiti wa kila mara kukagua wingi na mtawanyo wa samaki ziwani.

Anasema, mara ya mwisho utafiti mkubwa ulifanyika 1995 (miaka 24)



Ofisa Utafiti Mwandamizi, Athanasio Mbonde, akiwa na wenzake katika maabara inayotumika kuangalia utafiti wanaofanya. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

> **Hapo kinachofanywa ni ukaguzi wa chakula cha samaki, vimelea vya viroboto majini na virutubisho maji (mbolea) kama vile Naitrojeni na Fosiforasi na bakteria, katika athari zinazochangia kupungua samaki ziwani.**

na anasisitiza kuwa takwimu zake haziwezi kutumika sasa kuweka mipango endelevu katika uvuvi ziwani, kwani mabadiliko mengi yameshafanyika.

Hivyo, inasisitiza utafiti wa kila mara, hasa ikiangaliwa

Ziwa Tanganyika, linavyoathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi yanayopunguza wingi wa samaki na kuathiri mapato ya uvuvi.

Mkurugenzi huyo anafafanua kwa kina mazingira yanayoguswa ni tindikali majini, vumbi la madini tembo na taka, maji machafu kutoka mifumo ya vyoo, zote zina tafsiri ya upatikanaji samaki wa kutumiwa na umma.

Dk. Kimirei anasema wanajitahidi kufanya utafiti mbalimbali wa kijamii, kuhakikisha wanafanikisha malengo yao kuwa kituo bora cha utafiti, kinachonufaisha uwapo wa makazi ya samaki na kuishauri serikali hitaji hilo.

**Mafanikio**

Bosi huyo anasema ni miaka



Baadhi ya wavuvi wakiwa katika mwalo wa Katonga mkoani Kigoma wak katika Ziwa Tanganyika kuvua dagaa.**PICHA: MAELEZO**

# kupigania nganyika





ijiandaa kwa ajili ya kuingia

mitano sasa wamekuwa wakifanya utafiti kufuatilia athari za ongezeko la joto maji, dhidi ya uzalishaji na upatikanaji samaki aina ya dagaa na migebuka katika Ziwa Tanganyika.

Kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), iliyotoa baadhi ya vifaa vya maabara na boya waliloweka ziwani kupima kiwango cha joto na hali ya hewa kwa jumla.

Dk. Kimirei anasema, hilo boya ni la kwanza lenye uwezo mkubwa wa kukusanya takwimu za Ziwa Tanganyika na megine ya Afrika Mashariki na bara zima.

Anasema, utafiti huo na matokeo yake viliwezesha Tafiri na washirika wake kuandika pendekezo la sera lililowasilishwa kwa wizara husika na wadau wengine jijini Dodoma, Mei 6, mwaka huu.

Dk. Kimirei anasema wanashirikiana na Idara ya Sayansi za Maji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Aarhus nchini Denmark na Chuo Kikuu cha Illinois cha Marekani.

Mtazamo wake ni kwamba, itasaidia kiasi cha samaki kinachovuliwa kutumika chote na kubaki na ubora stahiki kwa muda mrefu.

Pia Dk. Kimirei anasema pamoja na ufadhili huo, Tafiri Kigoma kwa kushirikiana na Shirika la Matis la Iceland, walisambaza majiko bunifu 100 ya kukaushia samaki kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo wa Nchi za Unodi (Nordic Develoment Fund - NDF).

Anasema ni majiko yanayosaidia kupunguza uharibifu wa mazingira na kupunguza adha ya kinamama kuugua vifua, kwa sababu ya moshi wa kuni katika kuandaa samaki wao.

**Changamoto**

Dk. Kimirei anasema, changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni hujuma ya vifaa walivyowekeza ziwani na katika kipindi cha miaka minne boya limekuwa ziwani, vifaa vyao vimeendelea kuhujumiwa mara nyingi wakipoteza vifaa vyenye thamani kubwa.

Hata hivyo, anasema wamejitahidi kutoa elimu kwa jamii ili isiendelee kuharibu miundombinu husika. Anaongeza kuwa uongozi wa serikali nao umechukua hatua ya kupigania usalama wa chombo hicho.

Anataja changamoto nyingine ni kukosekana fedha za kutosha kufanya utafiti wa kila mara, hasa kuhusiana na wingi na mtawanyo wa samaki ziwani.

Pia anagusia kutokukubalika maombi ya ufadhili wa kufanyika utafiti, ili kupatikana taarifa sahihi kuhusiana na yanayotakiwa ziwani.

Dk. Kimerei analalamika kwamba, kuna uhaba wa watafiti waajiriwa na watumishi wenzao wa kada nyiginezo, kama vile mafundi mchundo, madereva, vitendea kazi vya kisasa, maabara na kompyuta.

Katika hilo, ushauri wake ni kwamba serikali inatoa kibali cha kuajiri watafiti na wafanyakazi wa kada nyingine, ili kuongeza ufanisi wa kazi za utafiti katika kituo hicho cha Tafiri Kigoma, ambayo eneo lake la kuhudumia ni kutoka Kigoma hadi Kasanga, Kusini mwa Ziwa Tanganyika.

Anafafanua, ni vigumu kuhudumia Ziwa Tanganyika kwa ufanisi yenye urefu wa kilomita 650, pasipo siyo kuwa na rasilimali watu, fedha za kutosha, na miundombinu kama maabara ya kisasa, magari na boti za kutosha.

Kwa mujibu wa Dk. Kimerei, kwa sasa kuna idadi ndogo ya wafanyakazi kulinganisha na jukumu zito la kuwajibika ziwani, hivyo anaiomba serikali kuangalia uwezekano kuongeza wafanyakazi wa Tafiri Kigoma.

Anasema, matarajio walio nayo ni kuandaa semina ya wadau wa uvuvi na uchakataji mazao ya uvuvi, kwa ajili ya kuwajengea uwezo utakaosaidia kupunguza upotevu wa mazao hayo ziwani.



Kapteni Yolanda Kaunda, akiwa na wasaidizi wake. Picha nyingine, watumishi wa ndege hiyo. **PICHA: MTANDAO.**

# Ndege ya wanawake pekee

UNAIKUMBUKA ndege ya wanawake pekee na tujiulize leo hii imefikia wapi? Rejea tangazo la siku ya Machi 15, mwaka 2017.

Hilo ni Shirika la Ndege Malawi, lilitangaza kuanzisha usafiri huo, chini ya Kapteni Yolanda Kaunda na msaidizi, Lusekelo Mwenifumbo.

Ni safari iliyopangwa kwa kuwa na marubani na wasaidizi wa abiria kwenye ndege wote wakiwa wanawake na ilipangiwa safari kati ya Blantyre na Dar-es-Salaam, ikipitia mji mkuu Lilongwe.

Taarifa kutoka kwa shirika hilo la ndege, lilisema lengo ni kufanikisha ulimwengu ambao 'unakumbatia jinsia zote.'

Mwenifumbo, aliyekuwa na umri wa miaka 24 wakati huo, alisomea taaluma yake mjini Addis Ababa, Ethiopia.

"Lengo la hatua hii ni kuwahamasisha wasichana ambao wangependa kufanya kazi katika uchukuzi wa ndege, lakini kwa njia moja au nyingine hufikiria ni vigumu au kwamba ni kazi ambayo wanawake hawaiwezi," taarifa ya Malawi Airlines, ilisema. Ni ndege aina ya Bombardier Q-400.



UCHUMI

# UPIMAJI KIDIGITALI WALETA MAISHA MAPYA UTAJIRI ARDHI MOROGORO

- Wajanja watumia kukopa bil.3/-
- Haki ya jinsia rasmi yajitokeza
- Uelewa wake ndio una safari
- Wafugaji walia kuenguliwa 'kiaina'

**Na Mashaka Mgeta, Morogoro**

SEHEMU kubwa ya wakazi vijijini nchini wanamiliki ardhi isiyopimwa na hawana hatimiliki zinazotambulika kisheria, hali inayochangia kukosekana fursa za kutatua migogoro ya mipaka, dhamana za mikopo na kushuka thamani ya rasilimali hiyo.

Kushamiri migogoro ya ardhi, kumeligharimu nchi hasara kubwa, ikiwamo hatua ya mauaji, mfano hai ni msuguano baina ya wakulima na wafugaji.

Ni takribani mwaka mmoja sasa, serikali kupitia msaada wa Sweden na Shirika la Misaada la Uingereza (UKaid), inatekeleza programu ya mfano wa kuwezesha umilikishaji ardhi (LTSP) katika wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, mkoani Morogoro.

Serikali inachuikua nafasi ya mratibu, mpimaji na mtoaji hati za kumiliki ardhi, huku asasi zisizokuwa za serikali kupitia 'mwamvuli' wa Tanzania Land Alliance (TALA), zimejumuishwa katika utoaji elimu, uhamasishaji na ufuatiliaji masuala mbalimbali yanayohusiana na ardhi na umiliki wake.

**UTATA ULIOPO**

Gualbelto Abdallah (45), ni mkulima kijijini Idunga, anayetetea mradi wa LTSP kuchochea ushirikishwaji jamii, inayotengewa maeneo ya mahitaji yao na kuwahakikishia umiliki, baada ya mpango wa kisheria wa matumizi bora, upimaji na michoro ya mipaka.

Pia, anasema upimaji huo wa kiteknolojia una athari za migogoro ya mipaka ya wananchi, pia baina ya vijiji.

"Utakuta kijiji fulani kina jiwe la mpaka wa siku nyingi, lakini walipokuja wapimaji ardhi wanaotumia tablet na satellite, mpaka uliokuwapo unahamishwa na kupelekwa kijiji kingine. Hapo ndipo mgogoro unapoanza," anasema.

Wakazi wa vijiji vinavyokabiliwa na migogoro hiyo, wanawalalamikia baadhi ya viongozi katika halmashauri ya wilaya hiyo, walihusika kupima mipaka ya awali, baadaye wamebadilisha.

"Kabla ya wataalamu kuja kupima ardhi, mipaka ya mwanzo ilikuwapo na iliwekwa, huku huyo mtumishi wa halmashauri akiwapo," anasema mwanakijiji wa Idunga kwa niaba ya wenzake na anaongeza:

"Walivyokuja kupima katika umilikishaji ardhi na huyo mtumishi akiwapo pia, mipaka ile ikabadilishwa."

Idunga ni moja ya vijiji vinavyokabiliwa na mgogoro baada ya upimaji na umilikishwaji ardhi. Inadaiwa ardhi yake imemegwa kupelekwa katika vijiji vya jirani vya Chikuti na Ikungua.

Ofisa Ardhi Wilaya ya Ulanga, Venance Huruma, anakiri kuwapo madai hayo, akiutafsiri ni kiashiria cha uelewa mdogo kuhusu upimaji uliofanyika.

Anafafanua vipimo vya awali vilitumia teknolojia duni iliyosababisha eneo kati ya kilomita nane na 10 kubaki wazi kati ya kijiji kimoja na kingine.

"Kwa hiyo tulipotumia teknolojia mpya na ambayo walistahili kuelimishwa kwa kina kabla ya upimaji, eneo lilibaki kuwa lile lile isipokuwa umbile likawa tofauti. Hapo ndipo dhana ya kuporwa ardhi ilipoibuka," anasema.

> **"Kabla ya wataalamu kuja kupima ardhi, mipaka ya mwanzo ilikuwapo na iliwekwa, huku huyo mtumishi wa halmashauri akiwapo," anasema mwanakijiji wa Idunga kwa niaba ya wenzake**



Mashamba ya wilayani Ulanga, yanavyoonekana kutoka angani. **PICHA: MTANDAO.**

**WAKOPA BILIONI 3**

Ofisa Ardhi mshiriki katika mradi wa LTSP wilayani Kilombero, Faraja Nkwere, anasema vijiji 58 kati ya 99 katika halmashauri hiyo vimepimwa na kumilikishwa hati zao.

Anasema, katika mpango wa serikali wilayani, umevihamsha vijiji 19 kuwa eneo la Kilombero mjini. Tayari hati zake zimeshadhamini

Sh. bilioni tatu, kwa mujibu wa taarifa za benki ya wakopaji.

Nkwere anaainisha takwimu wakopaji tisa wamenufaika, huku wengine wanakwepa kuisajili mikopo yao wakihofu.

Kijijini cha Idunga Wilaya ya Ulanga, kunasifiwa ni watunzaji vyanzo vya maji na wanazingatia taratibu za uhifadhi, pia usimamizi msitu uliopo.

Hapo kuna sheria ndogo zilizoanzishwa kuzuia shughuli za kibinadamu, pasipo idhini ya serikali ya kijiji.

Steven Zayumba, ni Ofisa Upimaji Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, anasema upimaji na umilikishaji ardhi ulichangia kupunguza migogoro ya rasilimali kwa jumla.

Hata hivyo, Zayumba anasema upimaji mpya umeibua migogoro, akitoa mfano wa vijiji vya Madibila na Kipenyo. Asili ya mgogoro ni eneo la mpaka wakazi wa Madibila wanaolalamika limehamishiwa Kipenyo.

**KINAMAMA NAO**

Taarifa mpya zinazotolewa ni kuibuka wanawake wanaomiliki ardhi, sambamba na vikundi vyao, mfano hai Kijiji cha Nkongo.

Pia, kuna ushuhuda familia iliyogawana sawa ardhi ya urithi pasipo kujali tofauti za kijinsia. Peter Mtetehenga, msemaji wa familia hiyo ya wanaume wawili na wanawake watatu, anaeleza namna jinsia ya kike ilivyowaongoza kufikia uamuzi.

Wakazi wa kijijini Majiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga,

INAENDELEA UK. 18



Mwanasheria kutoka Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Zarubaberi Ngowi (aliyesimama) akitoa mafunzo ya sheria zinazohusiana na masuala ya ardhi kwa wakazi wa kijiji cha Idunga wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# BIASHARA KATIKA PICHA




Meneja Mauzo wa Vodacom Tanzania Plc, Kanda ya Kaskazini, Straton Mchau, akizungumza katika hafla ya futari iliyoandaliwa na Vodacom kwa kushirikiana na benki ya Amana katika uzinduzi wa huduma mpya ya Halal Pesa ambayo inaendana na sheria za kiislamu ili kuleta faida kwa wananchi jijini Tanga hivi karibuni. **PICHA MPIGAPICHA WETU**



Mfanyakazi wa kampuni ya Milkcom wazalishaji wa maziwa na ya Dar Fresh akitoa elimu ya faida za unywaji maziwa katika maonyesho ya Wiki ya Unywaji Maziwa Duniani yaliyofanyika kitaifa, jijini Arusha mapema wiki hii. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Wachuuzi wakisubiri wateja na huku kukiwa na changamoto ya maji machafu yaliyosimama katika Soko la Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI



Sehemu ya mgawanyiko wa ardhi ya kilimo na msitu wilayani Kilombero. **PICHA: MTANDAO.**

# UPIMAJI KIDIGITALI WALETA MAISHA MAPYA UTAJIRI ARDHI MOROGORO

**INATOKA UK.16**

wanaelezea namna LTSP ilivyowapunguzia mapigano na kuchomana visu miongoni mwao.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Gothald Mitti anasema: "Kabla ardhi haijapimwa ulipofika wakati wa kilimo kulikuwa ni vita. Watu walichomana visu na wengine kukatana majembe wakigombea mipaka na mashauri hayo yalikuwa mengi kwenye serikali ya kijiji."

Ni msuguano unaoelezwa kukua zaidi kati ya kijiji hicho na Visegese, hali inayodaiwa kuchangiwa na mifumo ya utawala na siasa.

"Ilibidi mwaka 2014 tususie kufanya uchaguzi wa serikali ya kijiji kutokana na eneo letu kupelekwa Visegese, mpaka sasa hatuna viongozi wa kuchaguliwa," anasema Mitti.

**WAFUGAJI `WAFUNGUKA'**

Katibu wa Kikundi cha Wafugaji Nakafulu, Singu Manjale anasema upimaji na urasimishaji ardhi umesaidia kupunguza migogoro na kuondoa mapigano kati yao na wakulima.

Ni wafugaji kijijini wanaotajwa kuwa na kaya 35 zenye ng'ombe 1225, pasipo kujumuisha mifugo kama mbuzi na kondoo wametengewa eneo la hekta 70.5.

Inaelezwa eneo hilo dogo, ikilinganishwa na hesabu za kitaalamu zinazoelezwa kuwa ng'ombe mmoja anapaswa kufungwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta moja kwa mwaka.

Eneo la kijiji hicho ni takribani asilimia sita tu ya mahitaji, kwa ajili ya malisho ya ng'ombe waliopo humo.

Kumbukumbu za kijijini zinaonyesha awali eneo lilitengwa wakati kukiwapo kaya saba zilizomiliki wanyamakazi, lakini wakawavutia wafugaji kutoka nje na kusababisha ongezeko lililopo.

Singu ni eneo la wafugaji lisilo na miundombinu kama majosho ya kuogeshea ng'ombe na mabwawa ya kunywesha mifugo, hivyo kuathiri ufanisi katika malengo ya matumizi bora ya ardhi.

Anasema, eneo la majirani wa jamii hiyo ni wakulima wanaoishia mpakani, hivyo kushawishi kuibuka migogoro na mapigano.

"Mazao yanapolimwa eneo mpakani na mifugo haina mipaka ya kutembea, wakati mwingine unakuta imeshaingia kwenye shamba la mkulima," anasema Singu na kupendekeza kuondolewa mashamba mipakani.

Pia, upimaji na umilikishaji ardhi uliofanyika, umewaingiza wakulima kwenye eneo la wafugaji na wanaendelea na kufanya kilimo kinyume cha mpango wa matumizi bora ya ardhi.

**KUTOLEWA SHERIA**

Baadhi ya wakazi wa vijijini wameonyesha hawazifahamu sheria zinazohusiana na ardhi, hivyo kujikuta wanapoteza rasilimali hiyo au kufanya makosa yanayokatazwa kisheria.

Meneja Programu wa TALA, Jamal Omar, anasema wanavijiji wanahitaji kuelimishwa kuhusu sheria ya mazingira inayokataza ama ukataji, kusukuma au kuangusha mti, pasipo kibali cha mamlaka husika.

Omar anamfafanulia Magdalema Moyo, mkazi wa kijiji cha Idunda wilayani Ulanga, aliyetaka kujua sababu za kuzuiliwa uongozi wa kijiji hicho kutotumia miti miwili iliyoanguka shambani kwake.

> **"Mazao yanapolimwa eneo mpakani na mifugo haina mipaka ya kutembea, wakati mwingine unakuta imeshaingia kwenye shamba la mkulima," anasema Singu na kupendekeza kuondolewa mashamba mipakani.**

Jamal anasema, halmashauri za wilaya na vijiji zina miongozo inayotolewa na maofisa misitu kuwaelekeza wananchi kuhusu taratibu za kufuata inapotokea hali kama hiyo.

"Kwa mujibu wa sheria iliyopo, hata kama mti umeupanda mwenyewe, ukiukata pasipo kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa kijiji chako ni kosa la jinai.

"Pia, ukikutwa kwenye eneo la msitu pasipo ridhaa ya mamlaka husika ni kosa na faini yake si zaidi ya Sh. 50,000," anasema.

**MAKAZI MSITUNI**

Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji cha Idunga, Adelina Mpanda (45), anautaja mgogoro mwingine unahusu maeneo yaliyotumika kwa shughuli za kibinadamu, hasa makazi na kilimo 'kumegwa' kuwa sehemu ya misitu, ukiwamo Nampazi.

Pia, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inawaelekeza wanaolima kando ya mito kuondoka, hali iliyozua malalamiko na hisia za kukabiliwa na njaa.

Baadhi yao walilima mazao ya chakula; mahindi na ndizi kando mwa mto Luli na sasa wanatakiwa kusogea zaidi mita 60 kutoka kwenye kingo ya mto, hali inayoibua malalamiko kwa wakulima wanaodai kuathiriwa uzalishaji wa chakula na biashara.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Malinyi, Johnson, anasema wapo wanavijiji wenye maeneo yaliyopimwa na kurasimishwa, lakini hawajajitokeza kuchukua hati, hofu yao ni kutozwa kodi ya ardhi na mashamba.

"Yanapotolewa matangazo ya kulipia kodi za ardhi na mashamba, watu wanachanganya na uchukuaji hati za ardhi, wanadhani sasa wanakwenda kulipa kiasi kikubwa cha kodi na kwa lazima," anasema.

**MIGOGORO YA ARDHI**

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Idunga, Bertha Mwenda, anasema baadhi ya vipande vya ardhi kijijini vilipimwa na watu wasiohusika na hivyo kusababisha pingamizi zinazoendelea kushughulikiwa na serikali katika ngazi ya wilaya.

Bertha, anasema kaya 10 kati ya 421 zilizopo kijijini kwake, zinakabiliwa na migogoro ya ardhi na kusababisha ardhi yao isipimwe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usuluhishi ya kijiji cha Nakafulu wilayani Ulanga, Laurencia Maundu, anasema ugumu wa majukumu yao unatokana na mwitikio mdogo wa wajumbe wanaoshindwa.

Anasema, hiyo inachangiwa na kuwapo maslahi ya pande mbili, kulitiliwa shaka tafsiri ya kuwapo upendeleo upande mmoja.

Maundu anasema, kukosekana taratibu za uwasilishaji shauri la mgogoro wa ardhi kumetokea kwenye maeneo tofauti, akitoa mfano wa kijijini hapo.

Inaelezwa kuwa, watu waliokuwa katika mgogoro wa ardhi kijijini hapo, walifikishana polisi pasipo kupitia baraza la usuluhishi na kisha walirejeshwa kwa agizo la polisi.

Mratibu wa TALA, Jamal, anafafanua hilo kupitia Sheria ya Ardhi Namba Nne na Sheria ya Ardhi ya Vijijini Namba Tano za mwaka 1999, zinazoelezea mfumo wa utatuzi kuanzia ngazi za msingi.

Sheria hizo zitaja chombo chenye mamlaka ya awali katika utatuzi ni Baraza la Ardhi la Kijiji, linalofanya usuluhishi pasipo kuhukumu.

"Lakini kwenye maeneo mengine ya vijiji tumekuta mabaraza haya yanatoa uamuzi unaoitwa hukumu. Hiyo si sahihi, kwa maana wao wanasuluhisha tu. Hakuna mshindi wala anayeshindwa," anasema.

Anasema inapotokea wahusika hawaafikiani, wanapeleka shauri upya Baraza la Ardhi la Kata nako likikosa muafaka, asiyeridhishwa na uamuzi anakata rufani kwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

**WAFUGAJI WATENGWA**

Ofisa Upimaji Ardhi Wilaya ya Malinyi, Steven Zayumba, anasema vijiji sita havijakamilisha kutenga maeneo ya kufuga, wakati vinne; Minazini, Ziwa Kuu, Ipera na Njiwa vindai hawawataki wafugaji.

Kwa mujibu wa sensa iliyotokana na uchapaji chapa wa mifugo mwaka 2016 hadi 2018, wilaya hiyo ilibainika kuwa na mifugo 130,048, wakati eneo lililotengwa kwa mifugo ni hekta 13,500.

Makadirio yaliyopo, ng'ombe mmoja anatumia hekta moja kwa mwaka mzima na ukubwa wa eneo la mifugo wilayani unatosheleza asilimia 10 ya mahitaji.

**OFISA MIFUGO**

Ofisa Mifugo Wilaya ya Malinyi, Frank Johnson, anasema changamoto zinazowakabili wafugaji nchini zinaweza kutatuliwa, kwa baadhi yao kutambuliwa kuwa wawekezaji, ili wapate maeneo kwenye ranchi za taifa.

"Tuna ranchi zenye maeneo makubwa yasiyotumika, sasa ingefaa wafugaji wenye kukidhi vigezo wapewe hadhi ya uwekezaji na kuyachukua maeneo ya ranchi zetu kwa ajili ya shughuli zao," anapendekeza.

Anasema wilayani Malinyi, mifugo inaingizwa 'kimya kimya' nyakati za usiku na msimu wa masika na kusababisha ongezeko hilo, katika kipindi barabara nyingi zimeharibika na vigumu kufanyika doria.

Pamoja na changamoto zake, Jamal anasema tathmini ya jumla inaonyesha kuwapo mafanikio makubwa katika utekelezaji wa LTSP.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kupitia simu(+255) 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.***

UCHUMI



Pierre Philippe Blanc; mshauri wa mradi wa ufugaji majongoo bahari, unaosimamiwa na FAO. **PICHA: BBC.**



Huyu ndiye jongoo bahari. **PICHA: MTANDAO.**

# Zanzibar yapanda ngazi kiuchumi kupitia uzalishaji jongoo bahari

- Inamfuata bingwa Afrika Madagascar
- Neema za mapato, ajira zagonga hodi
- FAO yaingia na 'mikono miwili' kuisaidia

UKIAMBIWA kuhusu ufugaji wa viumbe hai baharini wakiwamo samaki, moja kwa moja utahisi ni lazima shughuli hiyo ifanyike nje ya bahari, ziwani au mto.

Mtu anapotembelea Zanzibar hususan katika kisiwa cha Uzi, huko kuna shughuli adimu ya ufugaji wa majongoo bahari. Ni moja ya mradi mikubwa inaotarajiwa kuwa chanzo cha mapato, ajira visiwani.

Pia, ni fursa muhimu ya uhifadhi wa viumbe bahari ambao katika siku za hivi karibuni wanahofiwa kutoweka.

Zanzibar sasa inakuwa ni ya pili katika Ukanda wa Afrika kuanzisha ufugaji viumbe bahari, wakiwamo majongoo bahari.

Nchini Madagascar, kuna miradi ya namna hiyo iliyopiga hatua kubwa, ikiwamo kama kinachofanyika Zanzibar, suala la ufugaji majongoo bahari.

Utafiti wa awali wa Shirika la Misaada la Korea (KOICA) mwaka 2012, ulipendekeza kuendelezwa kwa sekta ya uvuvi, kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya vyakula vya mazao ya baharini.

Katika kuendana na mtazamo huo, inajenga dhana muhimu ya mfumo wa uchumi wa namna hiyo, unaoendana na kutetea baadhi ya viumbe hai bahari waliopo hatarini kutoweka.

Homoud Talib, ni Mkazi wa Kisiwa cha Uzi anayefuga majongoo bahari. Anasema, awali kabla ya kupatiwa stadi za ufugaji kutoka Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), kupitia ufadhili wa KOICA, hawakuwa na stadi za kuyafuga majongoo bahari, ambayo tayari yalishaanza kuwa adimu.

"Siye wala hatujui kabisa. Unaweza kufuga majongoo bahari, basi tukawa tunayachukua baharini, lakini baadaye yakaanza kuwa adimu. Lakini, kwa sasa sababu tunayazalisha wenyewe na uzazi wake mkubwa sana ni matumaini yangu kuwa idadi itaongezeka sana," anasema Talib.

Katika orodha hiyo ya wadau, mwingine ni Harusi Said Ally, mama anayejitambhulisha kaingia katika kazi hiyo ya kufuga majongoo bahari kutokana na hamasa aliyoipata kutoka kwa mumewe.

Anaunga mkono kwamba kazi hiyo imembadilishia maisha kuelekea katika heri zaidi, ingawaje namna ya kuitumikia imekuwa changamoto kubwa kwake.

> **"Siye wala hatujui kabisa. Unaweza kufuga majongoo bahari, basi tukawa tunayachukua baharini, lakini baadaye yakaanza kuwa adimu. Lakini, kwa sasa sababu tunayazalisha wenyewe na uzazi wake mkubwa sana ni matumaini yangu kuwa idadi itaongezeka sana," anasema Talib.**

Harusi anakiri maisha yamembadilisha sana, lakini wanalazimika kuamka usiku kwenda kuwahudumia majongoo yao kabla ya maji ya bahari kujaa katika eneo wanalofugia viumbe hao.

MTAALAMU VIUMBE

Said Juma Shabaani ni mtaalamu wa viumbe hai bahari na ufugaji wa majongoo kutoka Shirika la Chakula Duniani FAO, anaelezea tabia za majongoo bahari ambazo zinarahisha ufugaji wake na udhibiti hivyo kusalia katika eneo lile lile walipohifadhiwa.

"Majongoo bahari kwanza wao hawatembei,bali wanazama kwenye mchanga. Hivyo, ukimuweka mahala utamkuta hapo hapo vinginevyo ingelikuwa vigumu udhibiti wake," anaeleza.

Pierre Philippe Blanc, ni Mshauri Mkuu wa Mradi kutoka FAO, aliyebobea katika uzalishaji wa majongoo, anasema kuwa mradi huo uliopo kisiwani Uzi ni moja ya miradi mkubwa na unaweza kuleta mageuzi makubwa na fursa ya ajira ndani ya Zanzibar, hadi Ukanda wa Afrika.

Kuhusu kituo cha uzalishaji vifaranga vya samaki na viumbe hai wakiwamo majongoo bahari, anasema wana uwezo wa kuzalisha hadi ziada ya majongoo wadogo anaowaita kitaalamu kwa jina 'seeds' na kuwasambaza katika soko la kisiwani Madascar na maeneo mengine ya Ukanda wa Bahari ya Hindi, kunakohitajika.

Mradi huo unaoendeshwa kwa ubia wa wafadhili KOICA na FAO, hadi sasa una matarajio makubwa kwamba, huenda ukaleta mageuzi makubwa katika uchumi wa Zanzibar, kutokana na kuwapo soko kubwa la majongoo katika nchi za Bara Asia na Ulaya. BBC.



Kundi la wadau wa maendeleo wa sekta ya kilimo, wakimwangalia jongoo bahari, anayefugwa katika kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki, Zanzibar**. PICHA: FAO.**

UCHUMI



Mpaka wa ukuta wa Marekani na Mexico. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Mexico yaja juu kutikiswa na ushuru wa wahamiaji kutoka kwa Trump

**Na Mwandishi Wetu**

NI msuguano wa aina yake. Sakata la uchumi, linalobeba sura ya siasa ya uchumi. Suala la kuzuiana kuhusu wavuka mpaka hasa kutoka Mexico, kwenda Marekani, kila kukicha kuna jambo jipya linayobeba kauli za kisiasa za wakubwa.

Ni jana, Radio ya Marekani, VOA inamnukuu Rais Donald Trump, akitamka kwamba maendeleo yameweza kupatikana katika mazungumzo kuhusu suala la ushuru ambao Marekani inatishia kuiwekea Mexico, ili kuiadhibu.

Adhabu hiyo inayozungumzwa ni kuhusu wimbi la wahamiaji wanaovuka mpaka kutoka Mexico, kwenda Marekani na kuzaa msuguano wa kisiasa.

Rais huyo wa Marekani, anasema hata maendeleo yaliyopo katika mazungumzo hayatoshi na anatishia kwa mara nyingine, kutoza ushuru wa asilimia tano aliyokusudia kwa bidhaa zote zinazotokea katika nchi jirani za kusini, pindi serikali ya Mexico, ikishindwa kuchukua hatua zinazostahiki dhidi ya wahamiaji.

Ni aina ya msuguano, lakini wenye sura tofauti na ile ya Marekani na China, ambayo imebeba sura zaidi ya ushuru. Mara zote, silaha kuu ya Rais Donald Trump ni ushuru.

Kiuchumi, ushuru kwa Mexico unaelezwa unaweza kuziathiri kampuni za Ujerumani kama vile watengenezaji wa magari Volkswagen, BMW na Daimler ambazo zinafanya uzalishaji nchini Mexico.

Huku kukiwapo kauli hiyo ya mkuu wa nchi ambaye anakamilisha ziara yake nchini Uingereza, yenye simulizi nyingi tata kuhusu siasa ya kiuchumi, tangu apokewe huko, awali serikali ya Marekani ilitamka kwamba hatua za Marekani ni kutekeleza madai yake dhidi ya Mexico.

Serikali ya Marekani inasema, vinginevyo jirani huyo anapaswa kujitathmini na vikwazo, kwani Mexico uchumi wake unaitegemea Marekani zaidi kutokana na ujirani iliyo nao na mfumo wa mitaji katika nchi hiyo.

Katika taarifa yake, Marekani inasema viwanda vingi vilivyoko Mexico ni vya Wamarekani, Wajapani na Wakorea, pia wanaotoka Ulaya, hatua iliyofanywa kuwapata watumishi wa bei nafuu, huku wakiuzia tena Marekani bidhaa za viwanda hivyo.

Inasema, Mexico haiwazuii wahamiaji lukuki kwenda Marekani, kwa kuwa maofisa wa serikali wananufaika na kadhia hiyo wakipatiwa rushwa mipakani.

Inarejea matokeo kwamba, Mexico itaumia yenyewe kuliko Marekani ambayo itaumia kidogo tu, tena kwa muda mfupi, kwa sababu viwanda vingi vya Mexico vitahamia tena Marekani, ili kuendelea na uzalishaji na kuiacha hoi nchi hiyo.

Mexico yajibu

Katika kile kinachoonekana kukerwa na 'kijembe; cha Marekani, maofisa wa Mexico wameeleza kuwa nchi zote zitaumia kiuchumi na walipinga uwezekano wowote wa makubaliano ya nchi ya tatu, itakayowalazimu wanaotafuta uhamiaji Marekani kupitia Mexico kwanza, kuomba hifadhi nchini humo.



Mexico ilionya Jumatatu kwamba, kitisho cha Rais Donald Trump wa Marekani kuiwekea Mexico ushuru mpya wa bidhaa zake zinazosafirishwa kwenda Marekani, utaumiza uchumi wa nchi zote mbili na kusababisha wahamiaji zaidi wa Amerika ya Kati kusafiri kupitia Mexico, ili kufika Marekani.

Kwenye mazungumzo yaliyoanza Washington, maofisa wa Mexico walieleza kwamba wataweza kufikia kiwango fulani tu cha kutekeleza matakwa ya Rais Trump ya kuzuia msururu wa wahamiaji wanaopitia Mexico, ili kuepuka ushuru wa asilimia tano unaotarajiwa kuanza Juni 10.

Balozi wa Mexico nchini Marekani, Martha Barcena na Waziri wake wa Mambo ya Nje, Marcelo Ebrard,

walipinga uwezekano wowote wa makubaliano na nchi ya tatu, itakayowalazimisha wanaotafuta uhamiaji Marekani kwanza kuomba hifadhi Mexico.

Balozi wa Mexico nchini Marekani, Martha, anaeleza kwamba kuna kiwango cha juu kabisa watakachoweza kufikia katika majadiliano ambacho alikitaja kwa jina 'hadhi ya Mexico.'

Anasema ushuru huo wa Marekani, unaweza kusababisha msukosuko wa kifedha na kiuchumi, hivyo kupunguza uwezo wa Marekani kukabiliana na kumiminika wahamiaji nchini mwake.

*Kwa mujibu wa vyombo vya habari mbalimbali.





# Wataka kulipwa fidia kupisha ujenzi

**Na Nebart Msokwa,**
KYELA

ZAIDI ya wananchi 200 wa Mji wa Kasumulu, Kyela mkoani Mbeya, wanaotakiwa kuyahama maeneo yao kupisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha baina ya Tanzania na Malawi, wameiomba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuwalipa fidia ili waendelee na maisha yao ya kawaida.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi, wananchi hao walisema wizara hiyo imeshindwa kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kutaka walipwe fidia zao kabla ya Mei 31, mwaka huu.

Kutokana na kushindwa kutekeleza agizo hilo, walisema mpaka sasa hawajalipwa huku wakiwa hawatakiwi kuyaendeleza maeneo hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Mchungaji John Kyamba, alisema wamekuwa wakisubiri fidia hizo kwa muda mrefu bila mafanikio na kwamba baada ya agizo la Rais, walianza kupata matumaini lakini bado hawajalipwa.

Alisema wanashangaa agizo hilo la mkuu wa nchi kupuuzwa kiasi hicho, huku akilinganisha maagizo hayo na ya Mungu ambayo hayawezi kupuuzwa na mtu yeyote.

"Kwenye Biblia tunaamini kuwa kauli ya Mungu ndiye ya mwisho, sasa Tanzania mwenye kauli ya mwisho ni (Rais) Magufuli. Hakuna anayeweza kubadilisha hilo ndiyo maana tunashangaa kwa nini agizo lake limepuuzwa kiasi hicho?" Alihoji Mchungaji Kyamba.

Alimwomba Rais Magufuli kusikia tena kilio chao na awasaidie ili walipwe na wayahame maeneo hayo na kwenda kuanzisha makazi mengine, ili kituo hicho kiendelee kujengwa bila mgogoro huku akisisitiza kuwa wanaunga mkono mradi huo. Naye Neema Lyolo alisema wanachotaka kwa sasa ni kutendewa haki ya kulipwa fidia na kwamba hawahitaji migogoro na serikali hasa kwenye shughuli za maendeleo.

Alisema tangu serikali ilipotangaza kuyachukua maeneo hayo, iliwazuia kuyaendeleza hali ambayo inawafanya waendelee kuishi maisha magumu.

Neema alisema maeneo hayo yalishafanyiwa uthamini na kilichobaki ni kulipwa, lakini kwenye hatua hiyo, wanapigwa danadana mara kwa mara na sasa wanashangaa hata agizo la Rais limepuuzwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Hunter Mwakifuna, alisema amefuatilia suala hilo mpaka wizarani na kuahidiwa kuwa wananchi watalipwa fidia mwishoni mwa Juni, mwaka huu.

Alisema alipofika wizarani, aliambiwa kuwa kinachoendelea kwa sasa ni uhakiki wa majina ya wananchi wanaostahili kulipwa na kwamba walimhakikishia mpaka kufikia Juni 30, mwaka huu, uhakiki huo utakuwa umekamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, aliwataka wananchi hao kuendelea kuvuta subira kwa madai kuwa suala lao linashughulikiwa kikamilifu na kwamba litakapokuwa tayari watalipwa fedha zao.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Miraji Mtaturu, akishiriki chakula cha sikukuu ya Eid El Fitr na wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Ikungi, katika hafla iliyoandaliwa na viongozi wa serikali na dini wilayani humo, mkoani Singida juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia na ubovu wa barabara

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Kilambo, Kata ya Mwatenga, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuwaboreshea barabara, ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji.

Wakizungumza juzi na Nipashe kijijini hapo, wananchi hao walisema ubovu wa barabara hiyo unasababisha changamoto ya kuwasafirisha wagonjwa kwenda hospitali ya wilaya hali ambayo inahatarisha maisha ya wagonjwa.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Sonyela, alisema baadhi ya wajawazito wamekuwa wakijifungulia njiani wanaposafirishwa kwenda hospitalini kutokana na ubovu wa barabara, hatua inayowafanya kutumia njia za asili kusafiri.

Alisema hivi karibuni mjamzito mmoja alipoteza maisha alipokuwa anakwenda hospitalini na kwamba kutokana na usafiri kuwa mgumu, alilazimika kutumia usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda.

"Mama huyo alikuwa anapelekwa katika Kituo cha Afya, ili akasaidiwe, lakini akiwa njiani uchungu ulimzidi na mpaka anafikishwa katika kituo hicho alikuwa tayari ameshafariki dunia. Tunaomba barabara hii iboreshwe ili kuokoa maisha ya watu," alisema Sonyela.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Moshi Ambali, alisema amekuwa akifuatilia wilayani kuhusu ubovu wa barabara hiyo, lakini hakuna mabadiliko yoyote yanayofanyika.

Alisema mbali na wagonjwa kupata shida kusafiri, wananchi pia wanashindwa kusafirisha mazao yao kwenda sokoni kwa urahisi hali inayowafanya wakulima wasipate tija kwenye kilimo chao ambacho ndiyo shughuli yao kuu.

Kwa mujibu wa Ambali, hali inakuwa mbaya zaidi wakati wa masika kwa kuwa maji huwa yanajaa kiasi kwamba hakuna usafiri wa aina yoyote ambao huwa unatumika katika eneo hilo. "Nimekuwa nikiwafuatilia wenzetu wa Tarura (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini), ili watusaidie barabara hii lakini hakuna kinachoendelea. Tunamwomba Mkuu wa Wilaya atusaidie kuwaelekeza ili watutengenezee barabara hii ambayo ni muhimu sana," alisema Ambali.

Meneja wa Tarura wa Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Abdul Mfumbili, alikiri barabara hiyo kuwa mbovu na kwamba wanakusudia kuanza kuitengeneza Septemba, mwaka huu.

Alisema barabara hiyo haiwezi kutengenezwa wakati wa mvua kutokana na eneo hilo kuwa na maji mengi, hivyo akasisitiza kuwa watakapokuwa wanaitengeneza wataiwekea miundombinu ya kuwezesha maji kupita bila kutuama barabarani.

Aliwataka wananchi hao kuvuta subira wakati maandalizi ya kuitengeneza barabara hiyo yanafanyika, huku akiwataka kuwa walinzi wa miundombinu hiyo pindi itakapokuwa imetengenezwa.

# Watembea kilomita 40 kusaka huduma za afya

**Na Nebart Msokwa,** MOMBA

WAKAZI wa vijiji vilivyopo kwenye Kata ya Mkulwe, Momba mkoani Songwe, wanalazimika kusafiri umbali wa kilomita 40 kwenda kutafuta matibabu katika Kituo cha Afya cha Kamsamba kutokana na kata hiyo kutokuwa na kituo cha afya.

Kutokana na hali hiyo wananchi hao wameiomba serikali kuwajengea kituo cha afya katika kata hiyo ambacho tayari wameshaanza kushirikiana kwa kuanza kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi huo unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Wakizungumza na gazeti hili juzi, wananchi hao walisema wamekuwa wakipata adha hiyo ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya, huku wakidai kuwa kutoka katika Kata hiyo kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa iliyoko Vwawa wilayani Mbozi ni zaidi ya kilomita 120.

Mmoja wa wananchi hao, Stella Kamizi, alisema licha ya kutembea umbali mrefu kufuata matibabu hayo, wamekuwa wakitozwa fedha nyingi wanapolazwa katika kituo hicho cha Kamsamba.

Alisema wamekuwa wakitozwa mpaka Sh. 35,000, hivyo ikijumlishwa na gharama za usafiri na kula, wanajikuta wanatumia mpaka Sh. 100,000.

"Tumeamua tuanze ujenzi wa kituo cha afya ndani ya kata yetu na wananchi wote tumehamasika kutokana na umbali tunaosafiri kwenda kutibiwa Kamsamba ambako tunatumia muda mrefu njiani, hivyo tunahatarisha maisha yetu," alisema Kamizi.

Edmund Kulanga alisema kukosekana kwa kituo hicho cha afya katika kata hiyo na gharama zilizopo katika kituo cha jirani cha Mkulwe kinachomilikiwa na Kanisa la Katoliki, wamelazimika kutembea umbali mrefu zaidi kwenda kufuata matibabu.

Alisema kwa sasa wanashindwa kuendelea na ujenzi wa kituo chao kutokana na kibali cha ujenzi kucheleweshwa, hivyo kuiomba serikali kuwahisha kibali hicho.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Momba ambaye ni Diwani wa Kata hiyo ya Mkulwe, Mathew Chikoti, alisema changamoto hiyo ni ya muda mrefu kwa wananchi hao na ndio maana wamehamasika kushiriki ujenzi wa kituo chao.





# Mahenge apiga marufuku uingizaji mifugo Mzakwe

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amepiga marufuku uingizaji mifugo kwenye chanzo cha maji Bonde la Mzakwe na kuonya kuwa atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Dk. Mahenge alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizindua kampeni maalum ya usafi wa mazingira jijini hapa.

Alisema anazo taarifa kuwa wapo wananchi ambao wameanza kuingiza mifugo kwenye eneo hilo na hivyo kuhatarisha chanzo hicho cha maji.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu huyo aliwataka wafugaji na wananchi kulinda chanzo hicho ambacho ni muhimu na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu.

"Ni marufuku kwa watu kuingiza mifugo kwenye chanzo cha maji bonde la Mzakwe na kwa yeyote atakayebainika kuingiza mifugo hatua zitachukuliwa dhidi yake," alisema. Akizungumzia kampeni ya usafi, Dk. Mahenge alipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutokana na kusimamia suala la usafi wa mazingira kwenye masoko kwa kuhamasisha uwekaji wa bidhaa kwenye meza maalum kama kanuni za afya zinavyoelekeza.

Kwa upande wake, Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alisema mafanikio ya usafi kwenye masoko yanatokana na jitihada kubwa za usafi zilizowekwa kwenye masoko yote.

Aidha, alisema mafanikio hayo pia yamechangia kuwafanya wafanyabiashara kukidhi maelekezo ya kiafya na kuepukana na magonjwa ya milipuko ambayo husababishwa na mazingira kuwa chafu.

Ofisa huyo aliwataka wananchi kuhakikisha wanafanya usafi mita tano kwenye maeneo ya makazi na biashara ili kuweka mazingira safi.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao kwa kuzingatia maagizo ya halmashauri.

Alitaja maagizo hayo ni kutofanya biashara kandokando ya barabara ili kuepusha na ajali na usumbufu kwa watembea kwa miguu.

Naye Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu jijini humo, Dickson Kimaro, alisema kwa sasa jiji hilo limekuwa likikusanya tani 150 mpaka 180 za taka kila siku kwenye dampo la Chidaye.

Hata hivyo, alisema wanaangalia utaratibu kubadilisha mfumo wa uondoshaji taka na kwamba wametenga gari maalumu kwa ajili ya kuhudumia masoko ili yawe katika hali ya usafi wakati wote.



Watoto wakisherehekea Sikukuu ya Eid El Fitr katika Uwanja wa Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanafunzi watakiwa kutunza mazingira

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imewataka wanafunzi kutambua umuhimu wa kutunza mazingira na kutumia mifuko mbadala kwa ustawi wa afya na maendeleo ya kiuchumi.

Wito huo ulitolewa na Mkaguzi wa Huduma za Hali ya Hewa na Mazingira kutoka TCAA, John Mfungo, alipokuwa akitoa elimu ya mazingira kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege jijini hapa.

Mfungo aliwataka wanafunzi kujikita kwenye matumizi ya mifuko mbadala kwa kuwa ni rafiki wa mazingira.

Alisema TCAA inatoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira katika ukuaji na ustawi wa mazingira.

"Hatua hii ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani na lengo letu ni kuongea na wanafunzi pia tuone uelewa wao kuhusu utekelezaji wa sheria ya mazingira ambayo inazuia matumizi ya mifuko ya plastiki," alisema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Cassian Henry, alipongeza elimu iliyotolewa na TCAA na kueleza inasaidia kutoa uelimishaji kwa wanafunzi kwa kuwa ni kundi linalohitaji elimu hiyo zaidi.

"Taasisi zingine zinapaswa ziige mfano huu wa utoaji wa elimu ya mazingira, elimu hii inatakiwa iwafikie wanafunzi wote nchi nzima, hivyo taasisi zingine ziungane na TCAA,"

# Wataka gesi asilia haraka waitumie kwenye magari

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAKAZI wa Mkoa wa Dodoma, wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa kufikisha gesi asilia nchi nzima ili kuitumia kwenye magari.

Wakizungumza na Nipashe, juzi baada ya kushuhudia gari linalotumia gesi asilia badala ya mafuta ya petroli, walisema kuwa hatua hiyo itasaidia kuondokana na matumizi makubwa, hivyo kuimarika kiuchumi.

Mmoja wa wakazi hao, Joyce Joel, alisema anatamani kutumia gesi hiyo, lakini kukosekana kwa kituo cha kujazia gesi mkoa wa Dodoma anakwama kubadilisha mfumo wa gari lake.

Alisema endapo serikali itafanya mchakato huo itawasaidia wamiliki binafsi wa magari kutumia huduma hiyo ambayo inaonekana nafuu

zaidi. "Tunaiomba serikali kuharakisha ule mchakato wa kufikisha huduma ya gesi mikoani, ili wananchi waweze kunufaika nao hasa kwa matumizi ya

magari kwa sababu wengi tulio mikoani tunahitaji huduma hiyo," alisema. Kwa upande wake, Bernard Chuwa alisema pamoja na huduma hiyo kuwa nzuri, lakini kituo cha kujaza gesi ni kimoja na kipo Dar es Salaam jambo ambalo linawafanya watu washindwe kupata huduma hiyo.

Akizungumza kuhusu hali hiyo, Mratibu wa Mradi wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari (CNG Vehicle Project) kutoka DIT, Dk. Esebi Nyari, alisema

ili kuwafikia wananchi mikoani kwa kushirikiana na wadau wengine wana mpango wa kusafirisha gesi hiyo katika magari.

Alifafanua zaidi ya kuwa changamoto ya kuwafikia wananchi walioopo mikoani ni kubwa kwa kuwa serikali haijafikisha gesi katika maeneo

hayo, lakini wao wameona ni bora kuisafirisha kupitia magari.

"Kuongeza mfumo wa gesi kwenye magari tunalenga kufika hadi mikoani na mfumo huu kwa gari ndogo unaendesha kilomita 25 kwa kilo moja,

wakati petroli lita moja unaenda kilomita 13 na mtungi wa gesi wa kilo 15 unaujaza kwa Sh. 20,000, hivyo unaotumia gharama ndogo," alisema Dk. Nyari.

Dk. Nyari alisema malengo yao wanatarajia wafunge mfumo wa gesi katika magari ya wateja wasiopungua 4,000 kwa mwaka.





Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein, akitoa mkono wa Eid El Fitr kwa wazee wanaoishi katika Nyumba ya Serikali Sebleni, Wilaya ya Mjini Unguja Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Dk. Shein ataka utii wa sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewasihi wananchi kutii sheria za nchi, ili wageni wanaoitembelea Zanzibar nao waige mfano wao na hatimaye waendelee kuishi kwa hali ya usalama na amani.

Akizungumza juzi katika Baraza la Idd el Fitri kwenye ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni mjini Zanzibar, Dk .Shein alisema kuwapo kwa amani na utulivu nchini kumezidisha kupiga hatua za ufanisi za utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Aliitaja mipango hiyo ni kuwa MKUZA III (Mkakati wa Tatu wa Kupunguza Umaskini Zanzibar), Dira ya Maenedeleo ya 2020, Mpango wa Dunia wa Maendeleo Endelevu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

Dk. Shein alisema nchi inayothamini na kufuata misingi ya utawala bora, watu wake huwa na uvumilivu maalum wa kuishi pamoja katika jamii ya watu wenye imani tofauti za kidini na kiutamaduni.

Alisema watu wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla wamekuwa kigezo kizuri miongoni mwa nchi kadhaa duniani katika kuuendeleza ustaarabu wa uvumilivu tangu kale na dahari.

"Kwa hakika uvumilivu ni miongoni mwa sababu zinazotuepusha na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe nchini. Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa tunu hii, tutahakikisha tunailinda amani na usalama nchini mwetu kwa kila hali," alisema Dk. Shein.

Aidha, alisema wananchi wa Zanzibar wana wajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia kuwa na uchumi unaokua mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2018/19 uchumi ulikua kwa asilimia 7.1 kutoka 7.0 na mfumko wa bei uliendelea kushuka kutoka asilimia 5.6 mwaka 2017/18 hadi asilimia 3.9 mwaka 2018/19.

Katika kuimarika kwa uchumi, alisema makusanyo ya mapato yameongezeka na kufikia Sh. bilioni 6668.7 mwaka 2017/18 kutoka Sh. bilioni 181.48 mwaka 2010/11 ambayo ni sawa na ongezeko la mara 3.7.

Dk. Shein alisema pato la mtu binafsi ambalo lilikuwa Sh. 942,000 mwaka 2010, limeongezeka hadi Sh. 2,323,000 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 146.7.

Alisema makusanyo na utekelezaji wa mipango ya maendeleo inaleta matarajio ya kukua kwa uchumi kufikia asilimia 7.8 katika mwaka wa fedha wa 2019/20 na hapana shaka kwamba Zanzibar itafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020 kama ilivyolengwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020.

Pamoja na hayo, Dk. Shein alisema serikali haina uwezo wa kumpa kila mtu mmoja pesa za matumizi katika kuendeshea maisha yake ila humlipa kupitia huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi.

Alisema kila kiongozi kwa nafasi aliyo nayo itamlazimu asimamie ulipaji kodi pamoja na utoaji wa risiti na kuwataka wananchi kuendelea kushajiishana juu ya utoaji na uchukuaji wa risiti, ili kuhakikisha kwamba kila senti inayopaswa kukusanywa na serikali inakusanywa.

## Waziri ataka malezi mema watoto yatima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewaomba walezi wanaolea watoto yatima kujitahidi kuwalea vyema kwa kutegemea fadhila kutoka kwa mola wao.

Waziri huyo alisema hayo juzi alipofanya ziara katika kituo cha watoto yatima cha Islah Center kilichoko Fuoni mjini Unguja.

Riziki alisema endapo watawalea vyema watoto yatima na wao wataondokana na ukiwa wa kuondokewa na wazee wao.

Aidha, aliwataka watoto hao kujitahidi katika masomo na kutosahau kuwaombea dua wazazi wao waliokwishatangulia.

Hata hivyo aliwaomba Waislamu nchini kuwasaidia watoto yatima kwa hali na mali ili nao wajihisi kama wako na wazazi wao.

Kwa upande wao, watoto yatima wa kituo hicho, walimshukuru waziri huyo kwa kufika kuwatembelea pamoja na kuwapatia sadaka. Walisema sadaka hiyo imewafikia kwa wakati mwafaka.

Mama mlezi wa watoto hao, Zalha Abdallah Makame, alisema wamefarajika kwa kufika kwake na kuwapatia sadaka hiyo na kumuomba kutoishia hapo na badala yake aendelee kuwasaidia kila hali itakapomruhusu.

Watoto yatima 17 wanalelewa katika kituo hicho cha Islah Center chini ya uangalizi wa Zalha.

# Robo ya wanawake pekee wamiliki ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya kwamba asilimia 75 ya wanawake Zanzibar ndio watumiaji wakubwa wa ardhi, wengi wao hawamiliki ardhi hiyo.

Hayo yalisema jana na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, katika kikao kilichowashirikisha watendaji mbalimbali wa serikali, wanaharakati na masheha, kwenye ofisi za chama hizo, Tunguu mjini hapa.

Alisema hali halisi inaonyesha kwamba wanawake waliowengi Zanzibar hawamiliki ardhi kwa sababu mbalimbali ikiwamo mfumo jamii uliopo ambao hauoni haja ya mwanamke kumiliki ardhi.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mzuri alisema: "Hii inasababisha mara nyingi hata ile haki ya kurithi ardhi huwa haipatikani."

Alisema ingawa hata sheria zinazofuatwa katika sehemu nyingi Zanzibar ikiwamo Sheria ya Mirathi ya Kiislamu inayompa haki mwanamke kumiliki mali, suala la mirathi limekuwa na uzito kwa warithi kulitekeleza.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na hali hiyo, wanawake wamekuwa hawapati haki wanazostahili kupitia mirathi kisheria.

Dk. Mzuri alisema pia katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na sheria zingine zinazohusiana na ardhi, zimetoa haki ya kumiliki kwa Mzanzibari ambaye amefikia umri wa miaka 18 bila ya kujali jinsia.

Alisema takwimu zinaashiria kuwa wanawake wanaomiliki ardhi ni kati ya asilimia 20 na 25 tu.

Alisema Tamwa Zanzibar kuanzia mwaka 2016, imekuwa ikihamasisha upatikanaji wa haki ya ardhi kwa wanawake, lakini bado takwimu za wanawake kumiliki ardhi ni ndogo.

"Mfano mwaka 2017 na 2018 Tamwa ilihamasisha wanawake zaidi 700 kwa kuwajengea uwezo juu ya umuhimu wa ardhi, kuwashauri kununua na kufuatilia haki za urithi na usajili," alisema.

# Benki yashiriki usafi mazingira

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

BENKI ya Akiba Commercial Bank tawi la Mwanza imetoa vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi pamoja na kufanya usafi katika Soko Kuu jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo Meneja wa benki hiyo tawi la Mwanza, Harriet Bujiku, alisema wanathamini mazingira na pia ni mdau mkubwa katika harakati za kuyatunza kwa kuwa hata sera ya huduma za kijamii imeweka kipengele cha mazingira kama sehemu mojawapo ambayo benki inashughulikia katika kurudisha sehemu ya faida yake kwa jamii inayohudumia.

"Sisi benki ya Akiba tumefarijika kupata fursa ya kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani inayoadhimishwa kila mwaka Juni 5, kwa kufanya usafi katika soko kuu la Jiji la Mwanza ambalo ni kubwa na linapokea bidhaa nyingi kutoka maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa," alisema na kuongeza:

"Tumetoa vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi vyenye thamani ySh. milioni tatu, ikiwamo mapipa ya kutunzia taka18, toroli mbili, koreo tatu,mifagio 18,buti jozi 12,glovisi jozi 13 na reki nne."

Bujiku alisema,wametoa vifaa hivyo, ili kuhakikisha soko hilo linakuwa safi, ikizingatiwa kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema 'kupinga uchafuzi wa hewa' ambapo benki hiyo inaunga mkono kwa kutambua umuhimu wa hewa safi.

Alisema, takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 92 ya watu duniani hawavuti hewa safi zinazohitajika, hivyo jitihada za makusudi kwa ajili ya kupambana na tatizo hilo lifanyike ili kulinda afya za watu, viumbe hai wengine na mazingira kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, aliipongeza benki hiyo, huku akiutaka uongozi wa soko hilo na Kata ya Pamba kuhakikisha wanatumia vifaa hivyo katika usafi sambamba na kuvitunza.

"Viongozi wa soko mtunze vifaa hivyo ili vidumu kwa kuwa mmepata bahati, kuna masoko zaidi ya 18 jijini hapa ila benki ya Akiba ikaona bora iwape nyinyi, lakini pia tunaendelea kusisitiza acheni matumizi ya mifuko ya plastiki kwani ukikutwa nayo ni sawa na umekutwa na meno ya tembo," alisema.

Aliongeza: "Adhabu yake utatoa faini ya Sh. 30,000 na kifungo, kwani mifuko hiyo haiozi pale dampo la Buhongwa kuna mifuko tuliyofukia miaka 35 iliyopita, lakini haijaoza na ukienda kuifukua unaikuta ipo na rangi yake na ilivyo na roho ngumu hata ukiichoma moto bado yanabaki masalia ambayo nayo hayaozi."

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Mwanza, Hamad Nchola, alishukuru benki hiyo na kuwataka wafanyabiashara kudumisha utamaduni wa kusafisha mazingira yote yanayowazunguka ili kuepuka maradhi.

# Viwanja vya taasisi wadaiwa kodi ya pango sasa kuuzwa

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imetishia kuwa itafuta milki na kuuza viwanja vya taasisi na mashirika, kampuni za umma na binafsi zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi, endapo wahusika hawatafika kwenye kikao kinachofanyika Jumanne ijayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Jumatano ya wiki hii na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dorothy Mwanyika, kikao hicho kimeitishwa na Waziri wa Wizara hiyo, William Lukuvi, kitakachofanyika Dodoma.

Mwanyika alisema taasisi na mashirika, kampuni za umma na binafsi pamoja na wenye maeneo ya viwanda na biashara yanayodaiwa kodi ya pango la ardhi na yenye malimbikizo ya muda mrefu wanatakiwa kuhudhuria kikao hicho ambacho kitafanyika siku hiyo kuanzia saa tatu asubuhi kwenye ukumbi wa Hazina.

"Mashirika, taasisi na kampuni yanayodaiwa kodi hii ya pango la ardhi na malimbikizo yanapaswa kufika yakiwa na nyaraka za umiliki pamoja na stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika," alisema.

Mwanyika alisema wadaiwa watakaoshindwa kufika kwenye kikao hicho, hatua za kufuta milki zao na kuuza viwanja husika zitafuata kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (sura 113) kifungu cha 50.

"Majina ya taasisi, mashirika na kampuni husika yameorodheshwa. Kwa wadaiwa wengine, ofisi zote za ardhi nchi nzima zitakuwa wazi siku zote pamoja na siku za Jumamosi na Jumapili hadi Juni 30 kwa ajili ya kwenda kuhakiki na kulipa," alisema.



Takataka za plastiki zikiwa zimerundikana na kuziba katika daraja la Mto Ng'ombe, eneo la Kinondoni Mkwajuni, jijini Dar es Salaam jana, jambo linalofanya maji kushindwa kupita vizuri na kusababisha mafuriko hasa nyakati za mvua. **PICHA: JOHN BADI**

# Soko la ghorofa la kisasa kujengwa kwa bil. 23/-

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 23 kwa ajili ya ujenzi wa soko kuu jijini Mwanza unaotarajiwa kuanza mwezi Agosti, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo litakalojengwa kuendana na hadhi ya jiji hilo.

"Kuanzia mwezi Julai na Agosti Mungu akituweka hai hapa habari yake ndefu... tunabomoa soko lote halafu linajengwa soko la kisasa la Sh. bilioni 23, tulishatangaza zabuni na mzabuni alishapatikana tunasubiri mikataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikirudi tusaini shughuli ianze," alisema Kibamba.

Alisema soko hilo la ghorofa mbili lenye eneo la maegesho ya magari zaidi ya 500 kwa wakati mmoja, vyumba vya maduka zaidi ya 500 na vizimba 1,500 litajengwa kwa muda wa miezi 18.

Soko hilo litakapokamilika watakaopewa kipaumbele ni wale waliokuwapo awali pia litakuwa na sehemu ya wafanyabiashara wadogo kufanyia biashara zao.

Aidha, Kibamba alisema Nyegezi itajengwa stendi ya kisasa ya ghorofa mbili yenye ukubwa mara nne ya iliyopo sasa ambayo itagharimu Sh. bilioni 14 na pembeni kutajengwa soko na sehemu ya wafanyabiashara wadogo pamoja na huduma za kifedha.

Pia kutakuwa na mradi wa ujenzi wa stendi ya kuegesha magari makubwa karibu na dampo la Buhongwa utakaogharimu Sh. bilioni 13.

Mwenyekiti wa soko kuu, Hamad Nchola, alimuomba mkurugenzi huyo kuhakikisha kuwa mzabuni anafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha kazi kwa muda wa mwaka moja tofauti na miezi 18 iliyopo kwenye mkataba.

## Umoja wa Mataifa wahofia ukame Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema nchi ya Somalia inakabiliwa na baa la njaa kwa sababu ya hali ya ukame ambao umekuwa ukishuhudiwa katika maeneo mengi ya nchi hiyo kwa muda mrefu sasa.

Mark Lowcock anayehusika na masuala ya kibinadamu UN, alisema hali iliyopo kwa sasa nchini Somalia ni mbaya, na haijawahi kutokea katika kipindi cha miaka 35.

Lowcock anaomba wahisani kusaidia kupatikana kwa Dola za Marekani milioni 45, ili kusaidia kupatikana kwa majisafi ya kunywa, chakula na mahitaji mengine ili kuwasaidia zaidi ya watu milioni mbili.

UN inasema watu wengine milioni 3.2 wanatarajiwa kukabiliwa na baa la njaa katika siku zijazo iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa, kwa sababu hali inaendelea kuwa mbaya.

Mbali na msaada huo wa dharura, UN unaomba Dola za Marekani bilioni 1.09 kusaidia kukabiliana na hali hiyo mwaka huu, lakini ni asilimia 22 ya fedha hizo ndio iliyopatikana.

Tangu mwaka 1992, Somalia imekuwa ikikumbwa na ukame kwa sababu ya kiwango kidogo cha mvua.

**RFI**

## Wahamiaji haramu 150 kutoka Afrika wakamatwa

**WASHINGTON, Marekani**

MAOFISA wa Marekani wanaolinda doria mpakani wamewakamata wahamiaji zaidi ya 150 kutoka Afrika wakijaribu kuvuka mpaka kinyume cha sheria kuingia mjini Texas katika mpaka wa kusini mwa Marekani.

Taarifa iliyotolewa na ofisi ya forodha na ulinzi wa mpakani (CBP) ilieleza kuwa idadi hiyo walikamatwa katika kipindi cha wiki moja.

Siku ya Jumamosi, maofisa hao walikamata kikundi cha wahamiaji haramu 37 kutoka Afrika ya Kati ambao walikuwa wamevuka mpaka eneo la Rio Grande wakiingia katika ardhi ya Marekani, CBP imesema katika taarifa yake Jumanne.

Ofisi hiyo imesema katika kundi hilo la wahamiaji kulikuwa na makundi ya wanafamilia, wakiwamo watoto wadogo, kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alhamisi iliyopita jioni, maofisa wa uhamiaji walikikamata kikundi cha wahamiaji kutoka Afrika cha watu 116 wakivuka mto kuingia eneo la Del Rio, CBP imesema katika taarifa yake ya Mei 31, 2019.

Kundi hilo ni la kwanza kwa ukubwa kukamatwa katika eneo la Del Rio, ofisi hiyo CBP imesema.

Eneo la mpaka wa Del Rio – Acuna liko takriban kilomita 260 (maili 160) ya mji wa San Antonio ulioko magharibi ya Texas.

**VOA**

# Umoja wa Afrika waipiga 'stop' Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

UMOJA wa Afrika (AU) umeipiga marufuku Sudan kushiriki katika shughuli zozote za muungano huo, hadi pale taifa hilo litakapounda serikali ya mpito inayoongozwa na raia.

Uamuzi huo unajiri baada ya AU kuwapatia watawala wa kijeshi wa taifa hilo siku 60 kukabidhi mamlaka kwa raia la sivyo wapigwe marufuku.

Onyo hilo lilijiri baada ya utawala wa jeshi nchini humo kupuuza makubaliano ya awali ya kujiuzulu katika kipindi cha siku 15 kilichoafikiwa na AU Aprili 15, mwaka huu.

Baraza la amani na usalama la AU lilisema kuwa lilijutia hatua ya jeshi hilo kushindwa kukabidhi mamlaka kwa utawala wa raia, hivyo linawapatia wanajeshi muda wa siku 60 kufanya hivyo.

AU ilisisitiza kuwa serikali ya kijeshi haitakubalika na matakwa, mahitaji ya taasisi za kidemokrasia na mikakati yake mbali na kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa raia wa Sudan.

Jeshi nchini Sudan lilichukua mamlaka baada ya kumpindua kiongozi wa muda mrefu Omar al Bashir kufuatia miezi kadhaa ya maandamano dhidi ya serikali.

Liliamua kufanya uchaguzi baada ya miaka miwili, lakini waandamanaji wamekataa uamuzi huo na kuamua kubaki katika barabara za Mji Mkuu wa Khartoum, wakitaka utawala wa kiraia.

Baraza hilo likiongozwa na Jenerali Abdul Fattah al-Burhan limekuwa likijadiliana na viongozi wa maandamano kuhusu uundaji wa serikali ya mpito. Lakini pande hizo mbili zimetofautiana kuhusu jukumu la jeshi ambalo limetawaliwa na wafuasi wa al-Bashir.

Wakati huohuo, maofisa nchini Sudan kwa mara ya kwanza wamekanusha madai kuwa watu 100 waliuawa na wanajeshi wakati wa maandamano na kukiri kuwa ni watu 46 waliouawa katika tukio hilo.

Madaktari wanaowatibia wananchi waliopata majeraha wanasema idadi ya watu waliouawa na vikosi vya usalama wiki hii imepanda na kufikia zaidi ya watu 100.

Walisema miili 40 iliopolewa kutoka mto Nile mjini Khartoum siku ya Jumanne.

Awali mamlaka nchini Sudan ilikuwa kimya kuhusiana na suala hilo, lakini maofisa wa wizara ya usalama walisema idadi ya watu waliofariki ni 46. Wanaharakati wa upinzani nchini Sudan wamekataa wito wa kufanya mazungumzo na baraza la kijeshi, wakihoji kuwa baraza haliwezi kuaminika baada ya kufanyika kwa ukaguzi dhidi ya waandamanaji. ***DW***



Wahamiaji haramu wakivuka kuingia Marekani kupitia njia zisizo rasmi. **PICHA: REUTERS**

# Maporomoko yaua sita, 50 wajeruhiwa

**KAMPALA, Uganda**

WATU zaidi ya sita wamethibitishwa kupoteza maisha na wengine 50 hawajulikani waliko baada ya kusombwa na maporomoko ya matope katika Wilaya ya Bududa, mashariki mwa Uganda.

Katika tukio hilo, nyumba zaidi ya 150, mifugo, na mimea vimefunikwa na matope, huku shughuli za uokoaji zikiwa zinaendelea.

Vijiji viwili vya Bunamwana na Bukobero, katika kata ndogo ya Buwali, wilayani Bududa, vimekumbwa na maporomoko hayo ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Msemaji wa Shirika la Msalaba Mwekundu, Irene Nakasiita, kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, aliandika kwamba maofisa waendelea na shughuli za uokoaji.

Mmoja wa mkazi wa kijiji cha Bunamwana, Nabende Wamoto, alieleza kuwa maporomoko hayo licha ya kuua yameacha uharibifu mkubwa.

"Hali ni mbaya, usafiri umeharibika na kwa sasa watu wenyewe wanafanya juhudi za uokoaji. Tunatarajia maofisa wa jeshi kutusaidia, lakini wametuacha kama tulivyo. Hali ni ya majonzi," alisema Wamoto.

Tukio hilo limetokea ikiwa imepita mwaka mmoja baada ya mto Suume kuvunja kingo zake kufuatia mvua kubwa na kusababisha maporomoko makubwa ya matope yaliyosababisha vifo vya watu 40.

Kijiji cha Bududa kinayopatikana karibu na mlima Elgon, kilomita 260 kutoka Kampala, mashariki mwa Uganda imekuwa sehemu hatari kwa makao ya watu kila msimu wa mvua, imekuwa ikikumbwa na maporomoko ya matope kila mwaka. Juhudi za serikali kuwahamisha watu kutoka sehemu zenye athari ya kutokea maporomoko ya matope hadi sehemu salama zimekosa kufaulu kutokana na ukosefu wa pesa. ***VOA***

# EID EL FITR KATIKA PICHA



Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (kushoto), akizungumza na waumini wa dini la kiislamu, baada ya kusherehekea nao sikukuu ya Eid El Fitr, katika kijiji cha Kome, jimboni humo, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**



Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mama Asha Suleiman Iddi akitoa mkono wa Eid El Fitr kwa wazee wanaoishi katika Nyumba za Wazee Sebleni, walipofika na Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein (hayupo pichani), kuwatembelea, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU Z'BAR**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mohammed Iqbal Noray, baada ya kushiriki Swala ya Eid El Fitr kwenye Msikiti wa Anwar, Msasani, jijini Dar es Salaam. **PICHA: OWM**



Sheikh wa Mkoa wa Kigoma, Hassan Kiburwa, akizungumza na waandishi wa habari kwenye Baraza la Eid El Fitr lililofanyika kwenye stendi mpya ya mabasi eneo la Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji. **PICHA: JOCTAN NGELLY**



Waumini wa dini ya kiislam wilayani Muheza mkoani Tanga, wakiwa nje ya msikiti mkuu wa Ijumaa, baada ya swala ya Eid El Fitr. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Wakazi wa Jiji la Dodoma, wakisherehekea sikukuu ya Eid El Fitri, kwa kupumzika kwenye uwanja wa Nyerere Square, jijini humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDAO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACEBOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33

## MCHANGANYIKO

**MONKALI INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu ya muda mrefu,inarejesha kongosho katika utoaji ute mchunguna kuwa normal balance 4.5.6 ipo ktk mfumo wa maji na vidonge husaidia mmengenyo wa chakula , tiba lishe, gaut, vidonda vya tumbo,bawasili, 0713293988/0758078280.

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

## GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR**
**LOW DENSITY AREA**
**BLOC "C",**
**PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

## NAFASI ZA KAZI

**MR SMART BARBERSHOP**

***Tunahitaji vinyozi wenye uzoefu na Wasichana wa kufanya huduma za saloon***

**kama scrub, mask n.k.**
Tuma ujumbe mfupi kwenda **0629 069 552**

**Tunapatikana kona ya Sanawari- Arusha.**

115262402

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223 311**

# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# VAN DIJK ATAKA MKATABA MPYA

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk ameiambia Liverpool anataka kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, kwa mujibu wa ESPN FC.

Beki huyo ghali zaidi duniani alisaini mkataba wa miaka mitano na nusu baada ya kujiunga na timu hiyo kwa ada ya uhamisho ya pauni mlioni 75 akitokea Southampton Januari mwaka 2018.

Virgil mwenye umri wa miaka 27 alikuwa na mchango mkubwa kwa Liverpool wakati ikishinda taji lake la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuifunga Tottenham mabao 2-0 mjini Madrid.

Na sasa beki huyo wa kimataifa wa Uholanzi anataka kuongeza mkataba mpya ili kuendelea kuwatumikia majogoo hao wa pale Anfield.

Wakala wa mchezaji huyo, Neil Fewings ameliambia gazeti la Daily Mail kwamba ana uhakika mteja wake atasaini mkataba mpya na klabu hiyo haraka itakavyowezekana.



# MADRID, CHELSEA WAKUBALIANA KUHUSU HAZARD

**LONDON, England**

HATIMAYE mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, amekamilisha mchakato wa usajili wake uliokuwa unasubiriwa kwa muda mrefu wa kujiunga na Real Madrid baada ya klabu hizo mbili kukubaliana kuhusu ada ya uhamisho wa nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atatia saini ya kuichezea Madrid inayonolewa na kocha Zinedine Zidane.

Uhamisho huo wa Hazard unakuja wakati akiwa ametoka kuisaidia Chelsea kubeba taji la Ligi ya Europa baada ya kushinda mabao 4-1 dhidi ya Arsenal.

Gazeti la Dail Mail limeripoti kwamba, ada ya Hazard itakuwa ni euro milioni 100 ambayo Real Madrid imekubali kuitoa.

Mara baada ya mchezo wa fainali ya Kombe la Ligi ya Europa, Hazard aliwaaga mashabiki na wachezaji wenzake kwa kusema kwamba, anafikiri hiyo ndio itakuwa mara ya mwisho kuichezea Chelsea.

Usajili huo wa Hazard unamaanisha kwamba miamba hao wa Santiago Bernabeu watakuwa wametumia kiasi cha pauni milioni 200, baada ya kumsajili Luka Jovic kutoka Eintracht Frankfurt kwa pauni milioni 57.7 na Éder Militão kutoka Porto kwa pauni milioni 44.

Madrid pia ipo kwenye mipango ya kutaka kumsajili Ferland Mendy kutoka Lyon, wakati Zidane akiwa anataka kuimarisha kikosi chake hicho.

Hazard amechezea Chelsea kwa kipindi cha misimu saba na amefunga mabao 110 katika mechi 350 alizowachezea Blues hao.

# Ronaldo amuita Sarri Juventus

**TURIN, Italia**

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, amesema yuko tayari kufanya kazi na kocha, Maurizio Sarri.

Kocha huyo wa Chelsea anahusishwa na mpango wa kujiunga na Juventus majira ya kiangazi.

Sarri mwenyewe ameweka wazi kwamba, anataka kuondoka hapo Chelsea baada ya kudumu nao kwa msimu mmoja.

Sarri anatarajiwa kutua Juventus wiki hii kujaza nafasi ya Maximiliano Alegri aliyeondoka baada ya kumalizika Ligi Kuu Italia msimu uliopita.

Awali, kulikuwa na utata kama nahodha huyo wa Ureno atafanya kazi na Mtaliano huyo kutokana na aina ya mfumo wake wa kufundisha soka.

Sarri alitengeneza safu imara alipokuwa kocha wa Napoli ambapo Gonzalo Higuain na Dries Mertens waliunda kikosi imara.

Vyombo vya habari Italia vimeripoti kuwa Ronaldo amekubali kufanya kazi na Sarri.

Napoli ikiwa chini ya kocha huyo, Higuain akiwa Juventus aliweka rekodi ya kufunga mabao 36 katika mechi 35 alizocheza msimu 2015/16.

Pia Mertens katika msimu huo, alifunga mabao 34 katika mashindano yota akiwa Napoli.

Ronaldo alimaliza vizuri msimu wake wa kwanza Juventus baada ya kuipa ubingwa wa Ligi Kuu Italia.






# ESPERANCE YATAKIWA KURUDISHA KOMBE

**TUNIS, Tunisia**

KLABU ya Esperance imetakiwa kurejesha Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika na kurudia kucheza mechi ya marudiano ya fainali.

Esperance ya Tunisia iliongoza kwa bao 1-0 kwenye mechi ya marudiano lakini wapinzani wao Wydad Casablanca waliondoka baada ya goli lao la kusawazisha kukataliwa.

Wydad walitaka video ya wasaidizi wa waamuzi VAR kuthibitisha kama lilikuwa goli au la, lakini mfumo wa mashine hiyo ulikuwa haufanyi kazi.

Shirikisho la Soka Afrika (Caf) lilisema kuwa mechi ya marudiano itachezwa katika uwanja wa ugenini.

Mechi ya marudiano itafanyika baada ya michuano ya Kombe la Mataifa Afrika itakayofanyika nchini Misri, itakayomalizika Julai 19 mwaka huu.

Taarifa ya Caf imesema taratibu za mchezo na usalama havikufuatwa kwenye mechi ya marudiano na kuweka wazi kuwa wachezaji wa Esperance lazima warejeshe medali za ushindi na kombe.

Mchezo wa marudiano uliingia dosari baada ya Waydad kufikiri kuwa wamesawazisha dakika ya 59 kupitia goli la kichwa la Walid El Karti. Mashine ya VAR ilionekana kando ya uwanja, lakini wachezaji hawakuelezwa kama ilikuwa haifanyi kazi.

Hatimaye mwamuzi akatoa ushindi kwa mabingwa mara tatu, Esperance baada ya dakika 95.

Rais wa Wydad amesema timu yake imeathirika na Caf ikaitisha mkutano wa kamati kuu ambao walitoa uamuzi wa kuwapo kwa mechi ya marudiano.



## Neymar kuikosa Copa America

**SAO PAULO, Brazil**

NEYMAR atayakosa mashindano ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, baada ya kuumia kifundo cha mguu juzi Jumatano wakati wa mchezo wao dhidi ya Qatar ambao walishinda 2-0.

Mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain aliwaacha Brazil kwenye majonzi baada ya kuumia kwenye mchezo huo wa kirafiki.

Neymar aliondoka uwanjani dakika ya 21 ya mchezo huo ambao Brazil waliibuka na ushindi, mabao yake yakifungwa na Richarlison na Gabriel Jesus.

Shirikisho la Soka la Brazil, lilisema katika taarifa yake ya jana Alhamisi kuwa, Neymar aliumia kifundo cha mguu na hataweza kupona na haraka na kushiriki michuano hiyo.

"Baada ya kuumia kifundo cha mguu wa kulia katika mchezo dhidi ya Qatar, Neymar alifanyiwa uchunguzi na kwamba hataweza kushiriki michuano hii," ilisema taarifa ya shirikisho hilo.

"Kutokana na kuumia, Neymar hatakuwa na muda wa kutosha kuweza kupona na kushiriki mashindano ya Copa America.

"Kwa maana hiyo, benchi la ufundi la Brazil litaangalia mchezaji gani wa kurithi mikoba yake."

Kocha wa Brazil, Tite ana muda hadi Juni 13, mwaka huu, kutaja mchezaji atakayechukua nafasi ya Neymar mwenye umri wa miaka 27.




## Maradona aomba kazi United

**LONDON, England**

GWIJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Argentinna, Diego Maradona, ameamua kuweka wazi hisia zake juu ya kuitamani ajira ya kocha wa sasa wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer.

Maradona amebainisha kwamba yeye anaamini anaweza kuwa mbadala sahihi katika kiti cha kocha huyo pale Old Trafford.

Maradona ambaye hana mafanikio mazuri katika nafasi ya ukocha tofauti na kiwango chake enzi anacheza, ameeleza kuwa Manchester United ndio klabu pekee ya nchini England ambayo amewahi kuiota kuifanyika kazi.

Na amesema kama United watakuwa wanafikiria kutafuta kocha mwingine ni vema wakamfikiria yeye.

"Kama (Manchester United) wanahitaji kocha nafikiri mimi ni mtu sahihi wa kufanya kazi hiyo, kwani Man United imekuwa ni klabu ya England ninayoipenda kwa muda mrefu, lakini kwa sasa naweza kusema pia Manchester City," alisema Maradona akinukuliwa na gazeti la Dail Mail.

"Najua ni ngumu kubadili ila ni kwa sababu ya Aguero tunaongea sana na anacheza vizuri pale," alisema.

Historia ya Maradona katika nafasi ya ukocha haivutii licha ya baadhi ya klabu kumwamini na kumpa nafasi.

Hadi sasa Maradona amekaa katika klabu kwa muda mchache hadumu sana, kwa sasa akiwa na klabu ya Dorados anahangaika kwa msimu wa pili kuipandisha Ligi Kuu timu ya ambayo inashiriki Ligi Daraja la Pili nchini Mexico kwa sasa.

--------------------

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BUFFON ATANGAZA KUONDOKA PSG

●●●Aeleza hataisahau klabu hiyo ya jijini Paris na alivyofurahi kupata...

**PARIS, Ufaransa**

GOLIKIPA Gianluigi Buffon anatarajia kuondoka katika kikosi cha Paris St-Germain mara baada ya mkataba wake wa kuitumikia klabu hiyo utakapomalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Mchezaji huyo mkongwe kutoka Italia ambaye ana umri wa miaka 41, alijiunga na klabu hiyo Julai mwaka 2018 akiwa mchezaji huru, na akiwa hapo jijini Paris amecheza mechi 25 za mashindano mbalimbali na kufanikiwa kushinda taji moja la Ligue 1.

Mshindi huyo wa mataji tisa ya Ligi ya Serie A, alipokuwa na kikosi cha Juventus alicheza michezo 656 katika kipindi cha miaka 17 ambayo aliyodumu mjini Turin.

"Ninataka kuondoka nikiwa na furaha, nimefurahi pia kupata uzoefu mpya ambao hauna shaka umenisaidia kuimarika," alisema Buffon.

"Leo nafasi niliyoipata ya kufanya kazi nje ya Italia inafikia mwisho.

"Ernest Hemingway aliwahi kuandika kuwa, kuna sehemu mbili tu duniani ambapo watu wanaweza kuishi wakiwa na furaha: Nyumbani kwako na jijini Paris. Leo na siku zijazo, hii tayari imeshanitokea pia mimi: Kwa maana nyingine, Paris itabakia kwenye kumbukumbu zangu kuwa ni nyumbani... Allez Paris!"

Buffon, mchezaji ambaye ameichezea Italia mechi nyingi, amecheza michezo 176, alitangaza kustaafu katika kikosi cha timu ya taifa baada ya kushindwa kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia zilizofanyika mwaka jana nchini Urusi.

Hata hivyo, Buffon ambaye alishinda taji la Kombe la Dunia mwaka 2006 akiwa na Italia, hajawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amepoteza mechi tatu za fainali, mwaka 2003 akifungwa na AC Milan, wakati mwaka 2014 alipoteza dhidi ya Barcelona na mwaka 2017 timu yake ilifungwa na Real Madrid.

PSG iliishia katika hatua ya 16 Bora katika mashindano hayo msimu uliopita, ambapo waliondolewa na Manchester United.

"Siwezi kusahau namna ambavyo kila mmoja anavyojisikia fahari anapokuwa Paris St-Germain, kwa upande wa klabu na mashabiki, walifurahi kuona Gianluigi Buffon anavaa jezi zetu," Mwenyekiti wa PSG, Nasser Al-Khelaifi alisema.

"Kwa muda wote ambao amekaa hapa PSG, alijaribu kuonyesha uzoefu wake na namna wachezaji wa kimataifa wanavyotakiwa kuonekana na si tu kwa wachezaji wenzake, lakini pia katika maeneo mbalimbali ya klabu. Tutamkumbuka sana tabia na haiba yake hapa klabuni."

## KWA UFUPI

### HAZARD NJIA NYEUPE
CHELSEA imekubali kupokea ada ya pauni milioni 88.5 kwa ajili ya kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard (28) ambaye anatakiwa na Real Madrid. ***(Guardian)***

### PSG YAMWANIA DE GEA
PARIS St-Germain inajiandaa kuwasilisha ofa kwa Manchester United ili kumwania golikipa Mhispania David de Gea (28), kwa lengo la kuziba nafasi ya Mtaliano Gianluigi Buffon (41). (Times - subscription required)

### DIJK KUZEEKEA LIVERPOOL
BEKI wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Virgil van Dijk ambaye ana umri wa miaka 27, amesema anataka kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo ya Anfield. ***(ESPN)***

### POGBA AZUIWA UNITED
KLABU ya Manchester United imesema haiko tayari kupokea ofa yoyote kwa ajili ya kumtoa kiungo wake Mfaransa Paul Pogba ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Mail)***

### FERNANDES RASMI UTD
MABOSI wa Manchester United wanatarajia kutangaza kuwa wamekamilisha usajili wa kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ye Ureno, Bruno Fernandes (240, nyota huyo anakuwa mchezaji wa kwanza kusaini katika klabu hiyo kwenye majira ya joto. ***(Star)***

### DORTMUND, ARSENAL VITANI
KLABU ya Borussia Dortmund inaamini kuwa mshambuliaji wake Mjerumani Mario Gotze (27), atasaini mkataba mpya baada ya kuhusishwa na tetesi za kujiunga na Arsenal. ***(Bild, in German)***

### PRAET APEWA RUKSA
SAMPDORIA imemwambia kiungo wake Mbelgiji, Dennis Praet (25) ambaye anatakiwa na Arsenal, anaweza kuondoka klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto. ***(HLN, in Dutch)***

### JAGIELKA ATAKIWA CELTIC
BEKI na nahodha wa Everton, Phil Jagielka ambaye sasa ana umri wa miaka 36, ametajwa kutakiwa na klabu ya Celtic katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

### KENNY ANUKIA SCHALKE
SCHALKE wamesema kuwa wanataka kumsajili Jonjoe Kenny (22) ambaye pia anawaniwa na Burnley pamoja na Crystal Palace, huku ikisema kwamba beki huyo wa kulia wa Everton ameshatua klabuni hapo kwa mkopo. ***(Mail)***

### KABAK AGOMBEWA EPL
KLABU za Arsenal, Manchester United na Tottenham zote zimeweka wazi zinamwania beki wa Stuttgart na Timu ya Taifa ya Uturuki, Ozan Kabak (19) ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 13.2. ***(Express)***

### RONDON ANG'ARA SOKONI
FENERBAHCE imejiunga katika mbio za kumwania straika wa West Bromwich Albion, Salomon Rondon. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 pia anawindwa na Wolves na Newcastle ambayo aliitumikia kwa mkopo msimu uliopita. ***(Ajansspor, in Turkish)***

### UMTITI: SIONDOKI BARCA
BEKI wa Barcelona, Samuel Umtiti (25), amewaambia mabosi wake kuwa hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo katika majira ya joto, licha ya kuwapo kwa tetesi za Mfaransa huyo kutakiwa na Arsenal na Manchester United. ***(Marca)***

### DJENEPO KIMEELEWEKA
MABOSI wa Southampton wamekubali kulipwa kiasi cha pauni milioni 14 na Standard Liege kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Mali, Moussa Djenepo (20). ***(Daily Echo)***

HABARI MICHEZO

# BODI YA LIGI YAJIPANGA KUMALIZA VIPORO BARA

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Ligi Kuu nchini (TPLB) imesema kuwa inajipanga vema ili kuhakikisha suala la "viporo" katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao halijitokezi, ili isiwe kikwazo kwa baadhi ya timu kama ilivyojitokeza katika msimu uliomalizika, imeelezwa.

Tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) imeshaweka wazi kuwa timu zitakazoshiriki katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni Simba na Yanga wakati Azam FC na KMC FC zenyewe zitapeperusha bendera ya Bara kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Stephen Mguto, alisema kuwa wameanza maandalizi ya kuandaa ratiba mapema, hasa baada ya kupata taarifa kuwa mwakani Tanzania Bara itawakilishwa na timu nne katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mguto alisema kuwa wadau wa soka wasiwe na wasiwasi kuhusiana na ratiba mpya kwa sababu taarifa za ongezeko la timu zimewafikia mapema, hivyo watahakikisha wanatoa ratiba kwa kuzingatia mechi za kimataifa za klabu na Timu ya Tanzania (Taifa Stars).

"Tunajipanga yale yaliyotokea msimu uliomalizika yasijirudie, tutahakikisha hakuna viporo, timu mbili tulisumbua, timu nne si ndio tutasumbuka zaidi, tusipokuwa makini mambo yataharibika," alisema Mguto.

Aliongeza kuwa ratiba itakayotolewa haitakuwa mbaya kama ilivyokuwa ya msimu uliomalizika ambayo iliifanya Simba kucheza mechi nyingi kwa siku chache, ili msimu huo wa ligi umalizike kama ilivyopangwa.

Hata hivyo, uongozi wa Lipuli FC ya Iringa ambayo timu yao ilicheza fainali ya Kombe la FA Jumamosi iliyopita inalalamika kukosa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho, nafasi ambayo wamepewa KMC.

Ongezeko la timu kwa upande wa Tanzania Bara, limekuja baada ya mabingwa wa Ligi Kuu, Simba kufika katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.



Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, akimkabidhi bendera ya Tanzania, nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta kwa ajili ya kuelekea Misri katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019). **PICHA: TFF**

# Matola njia panda Lipuli

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa Lipuli FC ya mkoani Iringa, Selemani Matola, amesema kuwa bado hajafanya uamuzi ni timu ipi ataitumikia katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2019/20.

Matola, nahodha na kiungo wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ametajwa kutakiwa na KMC FC baada ya kocha wake Mrundi Etienne Ndayiragije kuwa njia moja kuelekea Azam FC.

Matola ameisaidia Lipuli FC kumaliza katika nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika hivi karibuni na kucheza fainali za Kombe la FA kwa mara ya kwanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Matola, alisema kuwa ni kweli KMC walimfuata na kumweleza nia yao ya kutaka kumpa mkataba mpya, lakini aliwataka wasubiri kwanza amalize mchezo wa Kombe la FA.

Matola alisema kabla ya kufanya uamuzi, anahitaji kuona klabu atakayoifanyia kazi katika msimu ujao inakubali kutekeleza mapendekezo yake ambayo yatakwenda kwanza kuboresha kikosi na vile vile kufanya maandalizi yanayotakiwa ili kuwa tayari kushindana.

"Bado sijasaini mkataba wowote, ni kweli KMC waliniita ili tukae mezani, nikawaomba wanipe muda kwanza mpaka msimu utakapomalizika, na hasa wakati huo akili yangu ilikuwa inawaza mechi ya Kombe la FA dhidi ya Azam," alisema Matola.

Meya wa Kinondoni, Benjamin Sita, alisema jana kuwa mazungumzo na kocha wao Ndayiragije ambaye mkataba wake umemalizika hayako katika nafasi nzuri.

"Tunaendelea na mazungumzo, lakini nafasi ya kubaki ni asilimia 30 na asilimia 70 anaondoka," alisema meya huyo.

Sita alisema kuwa wamejiandaa kupokea uamuzi wowote ambao atauchukua kocha huyo ambaye walimwajiri kutoka Mbao FC ya jijini Mwanza.

## Cassian arejea, amshukuru Makonda

**Na Romana Mallya**

MSANII wa nyimbo za injili, Pascal Cassian, ambaye alikuwa akisumbuliwa na tatizo la mfumo wa figo na kibofu cha mkojo, ametoa shukurani kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa kugharamia matibabu yake nje ya nchi.

Cassian ambaye ni mshindi wa shindano la Bongo Star Search (BSS 2009), alipata ajali Oktoba mwaka jana, mkoani Singida akitokea Kigoma katika shughuli zake za injili, alifika katika ofisi za kiongozi huyo kumweleza kuwa sasa hali yake imeimarika.

Msanii huyo alifika kuonana na Makonda akiwa ameambatana na mke pamoja na watoto wake wawili.

**Makonda aliamua kum saidia kijana huyo baada ya kuona taarifa zake kupitia mitandao ya ki jamii na kuagiza atolewe nyumbani na apele kwe Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na aliahidi kugharamia mat ibabu yake ndani na nje ya nchi.**

Mkuu huyo wa mkoa alimpatia Cassian fedha za matibabu za kwenda India, tiketi za ndege kwa watu watatu waliomsindikiza pamoja na za malazi kwa siku zote walizokuwa nchini humo.

Alimweleza Makonda kuwa kwa sasa amepona na anaweza kuendelea kufanya shughuli zake za kutafuta kipato kama alivyokuwa hapo awali.

Cassian aliondoka nchini Machi 21 mwaka huu, kuelekea India ambako alifanyiwa upasuaji ambao umeimarisha afya yake.

Akizungumza jana baada ya kupata ugeni huo, Makonda alimshukuru Mungu kwa kutenda miujiza kwa kijana huyo ambaye aliondoka nchini akiwa amebebwa, huku akiwa na mifuko ya kuhifadhi haja ndogo.

"Ninawashukuru watu wote waliomuunga mkono kwa kumuombea Pascal hadi ameweza kupona, ninawaomba Watanzania tuwe na moyo wa upendo na kusaidiana," Makonda alisema.

Mke wa msanii huyo, Getruda alisema kama familia, walikata tamaa kwa hali aliyokuwa nayo mume wake, lakini tumaini jipya lilikuja baada ya Makonda kuwahakikishia kuwa atasimama nao bega kwa bega hadi kupona kwake.

# Michezo

Ijumaa Juni 7, 2019

Nipashe





## Buffon atangaza kuondoka PSG

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix (kulia), akipiga mpira huku mchezaji wa Uswisi, Ricardo Rodriguez akishindwa kumzuia kufanya shambulizi hilo katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya iliyochezwa juzi usiku mjini Porto. Ureno ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# SAMATTA: TUTAFANYA MAKUBWA

●●●Ni kutokana na kufahamu ukubwa wa mashindano hayo ya Afcon...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars) kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Misri ili kuendelea na mazoezi kwa ajili ya kushiriki Fainali za Kombe la Afrika, nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, amesema wamejiandaa kwenda kufanya vema katika michuano hiyo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, baada ya kukabidhiwa bendera, Samatta, alisema kuwa wachezaji wote wanafahamu mashindano hayo ni makubwa na wanachotakiwa kukifanya kwenye michuano hiyo ambayo Tanzania ilishindwa kushiriki kwa miaka 39.

Samatta alisema kuwa wamesikia nasaha zote ambazo wamepewa na serikali kupitia Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Juliana Shonza na kusisitiza kwamba wanaahidi kutowaangusha Watanzania.

Nahodha huyo aliongeza kuwa wamejiandaa kwenda kupambana katika mashindano hayo, huku wakionyesha uzalendo wa kiwango cha juu kwa sababu wanahitaji kupata matokeo chanya kwenye mechi zote watakazocheza katika mashindano hayo.

"Kwa niaba ya wachezaji, tunashukuru kwa kuwa hapa nasi (Shonza), ...umetutakia kheri huko tunakokwenda, nafikiri ni mashindano makubwa kila mmoja anafahamu, lakini sisi kama wachezaji tunasisitiza muhimu ni kuwa na uzalendo, uzalendo tunao, tunawaahidi tunaenda kupambana kuhakikisha kufanya kitu kinachoipa sifa Tanzania na serikali hii ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli," alisema Samatta.

Aliwataka wadau wa soka nchini kuendelea kuwaunga mkono kwa muda wote watakaokuwa Misri wakishiriki fainali hizo kama walivyokuwa pamoja wakati wanasaka tiketi ya kwenda kwenye michuano hiyo ya mwaka huu.

"Ninawaomba mwendelee kuwa bega kwa bega na sisi kwa kipindi chote tutakachokuwa kwenye mashindano, ninatambua kwamba Watanzania wanapenda mpira ndio maana wanatupa sapoti, hivyo kazi yetu tuliyopewa tutaifanya kwa ukamilifu kwa kuwapa zawadi ya ushindi kwenye mechi zetu ambazo tutacheza kwenye michuano ya Afcon," Samatta aliongeza.

**NYOTA SITA KUTEMWA**

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi cha Stars kitaondoka nchini leo saa 11: 00 jioni kikiwa na wachezaji 32.

Ndimbo alisema kuwa wachezaji ambao watabaki nchini, walitarajiwa kujulikana baada ya kufanya mazoezi ya mwisho leo asubuhi.

"Bado kocha hajaweka wazi wanaobaki, amesema atawatangaza baada ya mazoezi ya kesho (leo) asubuhi," Ndimbo alisema kwa kifupi.

Wakati huo huo, TFF ilikanusha taarifa zilizosambaa kuwa, Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Wilfred Kidao, amesema kuwa beki wa kulia wa Simba, Shomary Kapombe, ameondolewa rasmi kwenye kikosi cha Stars kutokana na changamoto ya majeraha yanayomkabili.

Stars inayofundishwa na Mnigeria Emmanuel Amunike ipo Kundi C ikiwa na timu za Algeria, Senegal na Kenya, huku ikipanga kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya wenyeji Misri itakaofanyika Juni 13, wakati Juni 16 itavaana na Zimbabwe.

# Kigogo Yanga akosoa usajili

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika msimu ujao, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Yanga, Jonas Tiboroha, amewataka viongozi wa klabu hiyo kujitathmini upya kuhusu wachezaji iliyowasajili hivi karibuni.

Tiboroha alisema kuwa endapo Yanga wanahitaji kufanya vema katika mashindano hayo ambayo waliyakosa katika msimu uliomalizika, basi wanatakiwa wahakikishe wanajipanga upya katika kuimarisha kikosi chao.

Kiongozi huyo ambaye kura hazikutosha katika uchaguzi uliomweka madarakani, Mshindo Msolla, alisema kwamba muda bado upo wa kusajili wachezaji watakaoweza kutoa ushindani katika michuano hiyo na kuipa heshima klabu yao.

**"Kwa usajili waliofanya hivi sasa, inaonekana Yanga ilikuwa inaanza kuboresha kikosi chake, kama itakwenda hivi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sioni kama itafanya makubwa," Tiboroha alisema.**

Tiboroha ametoa kauli hiyo baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuongeza idadi ya timu shiriki ambapo sasa Tanzania Bara itawakilishwa katika michuano hiyo na timu nne, uamuzi huo ukichukuliwa baada ya Simba kufanya vema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Mbali na Simba, timu nyingine zitakazopeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho ni Azam FC na KMC FC zote za jijini Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >